SportPesa
CHEZA USHINDE SASA
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



## Serikali yatoa tamko Mtanzania kukutwa kirusi kipya

UKURASA 7



## MAMBO 10 USIYOYAJUA KUHUSU KOCHA RANGNICK

UKURASA 12


# Nipashe

Jumatatu Desemba 6, 2021 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA J

ISSN 0856 • Na. 0579786

www.ippmedia.com


www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper


### UAMUZI WA SAMIA

# Bunge nalo laanika 'uchafu' zaidi TPA

**Kigogo** PAC afichua mkataba uliojaa utata akiwa Marekani...

*Endelea ukurasa 2*



Mwonekano wa Barabara ya New Bagamoyo kutoka Morocco hadi Mwenge yenye urefu wa kilometa 4.3 iliyojengwa kwa njia nne kwa ufadhili wa Serikali ya Japan, baada ya kufunguliwa na Rais Samia Suluhu Hassan jana. **PICHA: IKULU**




Ofisa Mkuu wa Fedha wa Benki ya CRDB, Fredrick Nshekanabo (kulia), akifurahi na baadhi ya watoto katika tamasha maalumu lenye lengo la kuwajengea watoto utamaduni wa kuweka akiba wakiwa wadogo kupitia akaunti ya watoto ya Benki ya CRDB (Junior Jumbo Account) na kuwashukuru wazazi na walezi kwa kuwafungulia watoto akaunti katika benki hiyo. Tamasha hilo limefanyika kwenye viwanja vya Mlimani City, jijini Dar es Salaam, mwishoni mwa wiki. **NA MPIGAPICHA WETU**

## Chanjo tano za corona zilizoruhusiwa nchini

UKURASA 2

## Miradi mikubwa mitatu kuanza kwa kasi Dar

UKURASA 7

**MICHEZO** WACHEZAJI YANGA 'MZUKA DABI' JUU UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6

HABARI KITAIFA

# Chanjo tano za corona zilizoruhusiwa nchini

**Na Salome Kitomari**

TANZANIA imeridhia aina tano za chanjo zinazoruhusiwa Watanzania kuchanja baada ya kufanyika utafiti wa kujiridhisha ambayo ni salama na inaweza kutumika kwa kadri ya mazingira ya nchi.

Hayo yalisemwa hivi karibuni na Mratibu wa Tiba Asili, Tiba Mtandao wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsi, Wazee na Watoto, Dk. Liggyle Vumilia,wakati wa mafunzo ya siku mbili kwa wahariri kuhusu UVIKO-19 yaliyoandaliwa na shirika lisilo la kiserikali la CDEA kwa ufadhili wa Graca Machel Trust.

Chanjo hizo ni Johnson and Johnson (J&J), Modena, Sinovac, Pfizer na Sinopharm kati ya nane zilizopitishwa na Shirika la Afya Duniani (WHO) na kwamba nchi imeangaliza matakwa yake ya ubora na kupitisha hizo zitumike nchini.

"Chanjo zote zipo sawa, tulichofanya ni uchaguzi wa ipi inatufaa kwa mazingira yetu. Hadi sasa tafiti zinaonyesha wengi wanaochanja hawajaingia kwenye ugonjwa (UVIKO-19) kali," alisema Dk.Vumilia.

Alisema kazi ya chanjo kwenye mwili wa binadamu ni kuamsha na kuimarisha kinga za mwili na si vinginevyo, na kwamba wapo wanaosambaza taarifa hasi ikiwamo kwamba baadhi ya chanjo zimetengenezwa kwa vinasaba huku akisisitiza vinasaba vikiguswa binadamu hachukui dakika tano anakufa.

Alisema pia watu wametishwa kuwa watakuwa mazombi, jambo ambalo siyo kweli, huku akitolea mfano wa kampuni ya J&J ambayo watu wametumia bidhaa zake za mafuta ya kujipaka na poda za watoto kwa miaka mingi na kama kungekuwa na nia ya kuwaua au kuwaumiza watu wangeshapatwa na madhara miaka mingi sana.

Kuhusu chanjo ya Pfizer, alisema imeshaingia nchini na imehifadhiwa sehemu maalum kwa kuwa inatakiwa kuhifadhiwa kwenye nyuzi joto hasi 80 hadi 60 na kwamba uhifadhi wake ni gharama kwa kuwa inataka baridi muda wote.

Kwa mujibu wa Dk. Vumilia, ikianza kutolewa itakuwa kwa wanaoweka nafasi au wanaoomba kupewa kwa muda maalum na siyo kama nyingine kuwa utakwenda kwa wakati wowote.

"Pfizer uhifadhi wake ni gharama sana, hii haitachomwa kama J&J, itakuwa kama umetoa 'order's itapelekwa kwenye vituo vikubwa, tumeshaandaa miundombinu yote muhimu ya kuhifadhia," alisema.

Alisema chanjo ya J&J unapofungua dozi moja inatakiwa kuchomwa watu watano na kwamba kwa zipo ambazo lazima mtu achanje mara mbili na asipofanya hivyo afya itakuwa mgogoro kwa kuwa dozi inakuwa haijakamilika.

Kwa mujibu wa Dk. Vumilia, asilimia 60 ya Watanzania wakichanja itapunguza wingi wa ugonjwa, huku akitolea mfano wa nchi ya Uingereza ambao hawavai barakoa na wanaingia uwanjani kuangalia mpira bila tatizo, na kwamba ili uingie ni lazima uwe na cheti cha chanjo.

Naye Mwenyekiti wa Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala Tanzania, Prof. Hamis Malabo, alisema dawa za asili zina mchango mkubwa kwenye kutibu magonjwa ya mfumo wa hewa na mengineyo, lakini zinadharauliwa na kupuuzwa kutokana na usasa. "Cha ajabu dawa zote za hospitali zinatengenezwa kutokana na mimea, lakini tunapotaka kusema mmea fulani unatibu tunaambiwa hiyo si dawa sahihi. Asilimia 60 ya Watanzania hawaendi hospitali wanajitibu kwa dawa za asili," alisema Prof. Hamisi ambaye ni mgunduzi wa dawa ya COVIDO.

Hadi sasa Tanzania imepokea dozi 4,421,540 za chanjo ikiwa ni awamu ya kwanza ya J&J zilikuwa 1,058,400 ya pili 169,000 na tatu 115,200 na kufanya jumla ya 1,342,600 huku chanjo ya Sinopharm na Pfizer zilizopokelewa ni 2,882,545.



Mkurugenzi wa Radio One/ Capital Radio, Deogratius Rweyunga, akimkabidhi cheti mwanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Wasichana ya John Baptist, Alphonsina Fedrick, aliyefanya vizuri somo la Utunzaji wa Kumbukumbu za Vitabu vya Fedha (Book Keeping) kwa niaba ya Mkurugenzi wa IPP, Abdiel Mengi, kwenye mahafali ya 14 kidato cha nne, hafla iliyofanyika shule hapo mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam. Shule hiyo ilipewa mchango wa Sh. milioni 100 na aliyekuwa Mwenyekiti wa IPP, Hayati Dk. Reginald Mengi kwa ajili ya kujengea mabweni. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## UAMUZI WA SAMIA

# Bunge nalo laanika 'uchafu' zaidi TPA

**Na Mwandishi Wetu**

SIKU moja baada ya Rais Samia Suluhu Hassan kuivunja Bodi ya Wakurugenzi wa Mamlaka ya Bandari (TPA), Bunge limepongeza hatua hiyo, likisisitiza kuwa kwa miaka mitano mfululizo limepaza sauti kuhusu 'madudu' kwenye mamlaka hiyo pasi na hatua kuchukuliwa.

Juzi Rais Samia aliivunja bodi hiyo kutokana na ubadhirifu unaofanywa na kuisababishia hasara serikali, akiweka wazi kuwa upotevu wa mapato unachangiwa na mifumo kutokuwa madhubuti.

Akizungumza na Nipashe akiwa Washington DC, Marekani jana, Mwenyekiti wa PAC, Naghenjwa Kaboyoka, alisema kwa takribani miaka mitano sasa kamati hiyo imekuwa ikiagiza bodi hiyo kuhakikisha mifumo ya bandari inafanya kazi kwa ufanisi na inasomana lakini utekelezaji wake haujafanyika kwa ufanisi.

"Kinyume chake mifumo hiyo ambayo imeligharimu taifa mabilioni ya shilingi imekuwa haifanyi kazi vizuri na hivyo kutoa mianya ya upotevu wa makusanyo ya fedha za umma.

"Mikataba mibovu na yenye kutumia fedha nyingi imekuwa ikiligharimu taifa fedha nyingi. Kwa mfano mfumo unaotumika sasa hivi umeingiwa na bandari siku za karibuni na matapeli wa... (anataja nchi ya Afrika). Wenye mfumo huo wanatoka... (anataja nchi ya Ulaya) na wamesema utazimwa mwaka 2023, hautatumika tena.

"Sasa unajiuliza kwa nini tufunge mfumo kwa mabilioni ya shilingi ilhali tukitambua kwamba ndani ya muda mfupi utazimwa?" Kigogo huyo wa PAC alihoji.

Kaboyoka alimpongeza Rais Samia kwa uamuzi wake wa kuiwajibisha Bodi ya TPA na kuagiza taasisi za uchunguzi zichukue hatua dhidi ya wahusika.

Katika moja ya vikao vyake vya kupitia hesabu na utendaji wa TPA, PAC ilipokutana na viongozi wa mamlaka hiyo Agosti mwaka huu, iliagiza kujibiwa kwa hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) za mwaka 2019/20 kutokana na TPA kupata hati isiyoridhisha na mifumo yao kutokufanya kazi ipasavyo.

Katika kikao hicho, Kaboyoka alisema: "Mifumo haijakaa vizuri, tumewaambia Ofisi ya CAG watuletee taarifa za ukaguzi maalum uliofanyika ili kuwa na uamuzi sahihi.

"Bado inaonyesha hawa watu hawajafanya lolote, wanasuasua sana, hata wahasibu wao walionekana hawajui kazi maana hata maswali waliyoulizwa wameshindwa kujibu, tumewarudisha warudi tena baada ya siku 14."

Alikumbusha kuwa kamati hiyo katika vikao vyake vya awali, iliagiza TPA kurekebisha mifumo yake kutokana na kutosomana na inatumika vibaya na kusababisha upotevu wa fedha.

"Hii mifumo inasababisha upotevu wa fedha kwa kuwa vitu vyao havipo wazi, wanajua mifumo ikitengenezwa vizuri itakuwa na uwazi mkubwa, tunajua kwamba Bandari bado ipo kwenye asilimia 40 ya makusanyo ya fedha za mapato," alisema.

Makamu Mwenyekiti wa PAC, Japhet Hasunga, alisema katika kikao hicho kuwa Bunge lilitoa maagizo ya mifumo ambapo zaidi ya mwaka mmoja na nusu hayajatekelezwa.

"Imeonekana maagizo ya Bunge yamedharauliwa na hayajafanyiwa kazi na mifumo wanayoendelea nayo haina tija kwa taifa.

"Kwa hiyo, tunataka waje baada ya wiki mbili wakajipange waje na maelezo ya kutosha ya namna ya kuja na mfumo mzuri utakaokuwa na maslahi mapana ya taifa letu kwa kuzingatia umuhimu wa bandari katika nchi yetu," Hasunga alisema.

Katika hotuba yake ya juzi, Rais Samia alisema taarifa ya ukaguzi maalum wa kiuchunguzi wa mfumo wa Enterprise Resource Planning (ERP), uliofanyika Juni 2020 dhidi ya mamlaka hiyo na ripoti yake kutolewa Machi mwaka huu, ilionyesha kuna upotevu wa fedha nyingi zilizotumika kuajiri kampuni mbalimbali za kuanzisha mifumo ya kielektroniki ya ukusanyaji wa mapato ambayo haikutoa tija iliyokusudiwa.

Alitaja kampuni hizo ni; Soft Tech Consultant Ltd ambayo ilipewa zabuni ya Sh. milioni 694 na kulipwa Sh. milioni 600; Kampuni ya Twenty Third Centaury System iliyopewa kazi ya dola za Marekani milioni 6.6 na kulipwa dola za Marekani milioni 4.6 na mkataba kuvunjwa; na Kampuni ya SAP-East Afrika Ltd iliyopewa dola za Marekani 433,000 na mshauri elekezi binafsi alilipwa dola za Marekani 31,920.

## HABARI KITAIFA

# Samia aagiza madarasa yajengwe kwa ghorofa

**Na Jenifer Gilla**

RAIS Samia Suluhu Hassan, ameelekeza ujenzi wa majengo ya shule nchini ufanyike kwa mtindo wa ghorofa ili kuepuka adha ya uhaba wa maeneo uliopo.

Rais Samia alitoa maelekezo hayo jana katika sherehe za uzinduzi wa barabara ya Mwenge –Morocco yenye urefu wa kilomita 4.3 katika viwanja vya Chuo cha Ustawi wa Jamii jijini Dar es Salaam jana.

Maelekezo hayo ya Rais Samia yalitokana na hoja iliyoibuliwa na Mbunge wa Kinondoni, Abbas Tarimba ambaye alisema:

"Mheshimiwa Rais, Kinondoni tumepokea Sh. bilioni 3.3 katika zile fedha za Covid kwa ajili ya kujenga madarasa, maeneo ya hospitali...Kinondoni mimi nilihitaji shule mbili za sekondari, kata zangu mbili hazina shule za sekondari, Kata ya Tandale na Kata ya Kinondoni."

Rais Samia alisema tatizo la kutokuwa na maeneo ya kujenga shule limejitokeza zaidi ya mara moja, hivyo ni wakati sasa wa kubadilisha mtindo wa ujenzi.

"Na leo nalikuta sehemu ya pili, nilipokwenda Mkuranga nilikuta tatizo hili, ujenzi wa shule, lakini eneo halitoshi, nimelikuta tena hapa Kinondoni.... nadhani ni wakati mwafaka sasa tubadilishe ujenzi wa shule zetu, badala ya mabanda (majengo) kwenda kwa upana sasa yaende kwa juu (ghorofa), nadhani kwa eneo dogo tunalolipata tujenge kwa juu, ambako hakuna mipaka," alisema.

Kuhusu fedha za miradi, alisema serikali pia inakusudia kuimarisha tathmini ya ufuatiliaji wa fedha za miradi inazozitoa kwa kuajiri watathmini wa fedha hizo ili kufuatilia matumizi yake katika miradi.

"Nataka niseme kuwa fedha zile trilioni 1.3 (zilizotolewa na IMF) zinahitaji tathmini ya ufuatiliaji wa sasa hivi na halafu, sisi serikali kuu tuanze sasa kuimarisha kitengo cha tamthini na ufuatiliaji na muda si mrefu hatua mtazisikia ndani ya Wizara ya Fedha," alisema Rais Samia.

Aliishukuru Serikali ya Japan kwa misaada inayoendelea kuitoa kuboresha miundombinu ya barabara na madaraja na kuahidi kushughulikia changamoto walizokumbana nazo katika utekelezaji wa ujenzi huo ili isijirudie katika miradi ijayo.

Mhandisi Rogatus Hussein Maswila, Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara nchini (TANROADS), alisema mradi huu umegharimu jumla ya Sh. bilioni 71.9, wakati serikali ya Tanzania ilitoa msamaha wa tozo mbalimbali stahiki katika utekelezaji wa mradi zinazohusisha uhamishaji wa miundombinu na fidia zenye jumla ya Sh. bilioni 8.2.

Naye Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi , Prof. Makame Mbarawa, alisema ujenzi huu utapunguza ajali kwa watumiaji wake, nipende kuchukua fursa hii kuishukuru serikali na watu wa Japan, tunakushukuru sana Balozi," alisema Mbarawa.


**KUPOTEA KWA CHETI CHA USAJILI (CHAMA CHA WAKULIMA)**

**KUMBUSHO IDDI KIVIZA**

Anatangaza kupotelewa kwa cheti cha usajili cha chama cha wakulima umwagiliaji **mlali/kipera(c.u.m.k.i)** namba ya usajili, **no.12066,** kimepotea yeyote atakae kiona atoe taarifa kituo cha polisi au piga simu namba **0658365548**

**MOR/MOR/RB/574013/2021**

116600302



Ujamaa Community Resource Team

PO Box 15111, Arusha, Tanzania

www.ujamaa-crt.org

**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MIRADI.**

SHIRIKA LA UJAMAA COMMUNITY RESOURCE TEAM NI SHIRIKA LISILO LA KISERIKALI LINALOJISHUGHULISHA NA KUJENGA UWEZO WA JAMII KATIKA MASUALA YA UTAWALA BORA, ARDHI NA MAZINGIRA KATIKA MIKOA YA ARUSHA NA MANYARA.

SHIRIKA LINAPENDA KUUTANGAZIA UMMA KUWA LITATEKELEZA MIRADI MIPYA IPATAYO MITANO KAMA INAVYOAINISHWA HAPA CHINI KUANZIA DESEMBA 2021 MPAKA MWAKA 2022

1. UCRT KWA UFADHILI WA FOUNDATION OPEN SOCIETY INSTITUTE (FOSI)LITATEKELEZA MRADI WA "PROMOTE DEVELOPMENT OF EFFECTIVE AND ACCOUNTABLE LOCAL GOVERNMENT INSTITUTIONS FOR STRENTHERNING COMMUNITY LAND RIGHTSUTAKAOGHARIMU KIASI CHA DOLA ZA KIMAREKANI 50,000.00
2. UCRT KWA UFADHILI WA THE NATURE CONSERVANCE ITATEKELEZA MRADI UJULIKANAO KAMA ``AFR NORTHERN TANZANIA RANGELANDS `` KATIKA WILAYA YA SIMANJIRO NA MONDULI UTAKAOGHARIMU KIASI CHA SHILINGI ZA KITANZANIA 91,799,060.00
3. UCRT KWA UFADHILI WA UNOPS ITATEKELEZA MRADI WA MATUMIZI BORA YA ARDHI KWA WILAYA YA LONGIDO UTAKAOGHARIMU DOLA ZA KIMAREKANI $ 31,973.00

***MIRADI HII YOTE ITATEKELEZWA KWA KUSHIRIKIANA NA HALMASHAURI HUSIKA PAMOJA NA VIJIJI.***

**KWA MAWASILIANO ZAIDI director@ujamaa-crt.or.tzna manager@ujamaa-crt.or.tz**

116599702




Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Alphayo Kidata, akipokea tuzo ya ushindi wa kwanza katika kundi la Wakala wa Serikali kwenye Shindano la Uandaaji Bora wa Hesabu kwa Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Hesabu za Sekta za Umma kwa mwaka 2020. Shindano hilo liliandaliwa na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu Tanzania (NBAA), hafla hiyo ilifanyika Kituo cha Mikutano NBAA Bunju Dar es Salaam, juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

UIMARISHAJI WA USHIRIKIANO BAINA YA TANZANIA NA JAPAN

# Barabara mpya ya Bagamoyo, awamu ya pili, kielelezo kingine cha ushirikiano wa Tanzania na Japan

Maliki Muunguja

Ili nchi yoyote iweze kuchochea maendeleo yake ya kijamii na kiuchumi, inahitaji kuwekeza katika miundombinu yake.

Hii hufanya usafirishaji wa watu na mizigo kutoka sehemu moja hadi nyingine kuwa rahisi na nafuu.

Kumekuwapo ushirikiano wa Serikali kuu, Serikali za mitaa na mashirika ya ndani na ya kimataifa katika kuboresha hali ya sekta ya usafiri.

Shirika la Maendeleo la Japan (JICA) ni miongoni mwa washirika wakubwa wa ushirikiano wa maendeleo duniani, na limekuwa likitanua wigo wa ushirikiano wake kupitia njia mbalimbali kama vile ushirikiano wa kiufundi, mikopo ya masharti nafuu, misaada na wafanyakazi wa kujitolea wa Japani nchini Tanzania.

Kwa hivi karibuni, kwa kuongezea, JICA imetanua jalada lake la ushirikiano kwa kuwekeza fedha katika sekta binafsi.

JICA ina ofisi 96 duniani kote, 28 zikiwa katika nchi za Afrika zilizo katika kusini mwa jangwa la Sahara.

Tanzania ni miongoni mwa nchi hizo zinazofaidika na misaada ya maendeleo ya Japan miongoni mwa nchi hizo za kusini mwa jangwa la Sahara za Kenya, Ghana, Senegal na Zambia.

Kiwango cha msaada wa Japan chini ya JICA kwa Tanzania kupitia mpango wa ushirikiano (Shilingi Milioni*)

Ukuzaji wa miundombinu ya usafiri ni mojawapo ya sekta za kipaumbele za ushirikiano wa JICA, na inachangia takriban asilimia 27 ya jumla ya ushirikiano wa JICA nchini Tanzania.

Ushirikiano huo unachangia ukuaji jumuishi, endelevu na ustahimilivu, na kutokomeza umaskini kupitia ukuaji huo.

Kuendeleza miundombinu ya usafiri kunashughulikia malengo mahususi katika Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) kama vile Lengo la 9 "kujenga miundombinu thabiti, kukuza ujumuishi wa uendelevu viwanda, na kuchagiza uvumbuzi," Lengo la 11 "kufanya miji na makazi ya watu kuwa jumuishi, salama, imara na endelevu," na Lengo la 17 "kuimarisha njia za utekelezaji na kuhuisha ushirikiano wa kimataifa kwa maendeleo endelevu."

Ushirikiano wa JICA hauzingatii idadi tu bali pia ubora, kwani miundombinu duni inaweza kuzuia maendeleo ya nchi katika kipindi cha muda wa kati/mrefu.


Katika hali hii, JICA inaendesha miradi kwa mujibu wa "Kanuni za Uwekezaji Bora wa Miundombinu."

Kanuni hizo zilipitishwa katika Mkutano wa G20 wa Osaka Juni 2019, na zinaonyesha mwelekeo wa kimkakati wa kuchangia katika kuondoa tabaka lililopo katika sekta ya miundombinu, kuendeleza miundombinu kama nyenzo ya ukuzaji mali, na kuongeza athari chanya za uwekezaji wa miundombinu kulingana na hali ya nchi.

Zaidi, JICA inasaidia kuboresha muunganiko kati ya mabara mawili yanayokua kwa kasi ya Afrika na Asia kupitia Bahari ya Hindi na Pasifiki, tangu upitishwe mpango wa "Muunganiko wa Bahari za Hindi na Pasifiki huru na wazi" ambao umekuwa ufunguo wa ustawi wa kijamii na kiuchumi na maendeleo ya mabara.

*"Kanuni za Uwekezaji Bora wa Miundombinu" zilizopitishwa katika Mkutano wa G20 Osaka 2019*

1) *Kuongeza athari chanya ya miundombinu ili kufikia ukuaji na maendeleo endelevu*
2) *Kuongeza ufanisi wa kiuchumi katika mtazamo wa gharama ya mzunguko wa maisha*
3) *Kuunganisha masuala ya mazingira katika uwekezaji wa miundombinu*
4) *Kujenga uwezo wa kuhimili majanga ya asili na hatari nyinginezo*
5) *Kuunganisha masuala ya kijamii katika uwekezaji wa miundombinu*
6) *Kuimarisha usimamizi wa miundombinu.*



Muonekano wa juu wa barabara mpya ya Bagamoyo, awamu ya pili.



Ujenzi unaondelea wa barabara mpya ya Bagamoyo.

## Utatuzi wa changamoto ya msongamano Dar es Salaam

Juhudi zinafanywa kupunguza msongamano wa magari katika Jiji la Dar es Salaam ambalo ni kitovu cha biashara nchini.

Msongamano wa magari katika jiji la Dar es Salaam unatambulika kama moja ya vikwazo vikubwa vya ufanyaji biashara katika jiji hilo ambalo lina wakazi zaidi ya milioni 6.

Kwa mujibu wa Mpango Kabambe wa Usafiri wa Jiji la Dar es Salaam, barabara ya mpya ya Bagamoyo ni mojawapo ya barabara zenye msongamano mkubwa jijini, kikwazo kikubwa cha msongamano kikiwa ni wingi wa magari katikati ya jiji na maeneo yaliyo nje ya jiji. Ilitazamwa kama eneo la kipaumbele cha juu.

Dar es Salaam ni eneo nyeti kwa sekta ya usafiri. Ndiyo kitovu cha mifumo yote ya usafiri ikiwa ni pamoja na barabara, reli, usafiri wa anga na baharini. Ni eneo lenye tija kwa usafiri nchini Tanzania.

Katika kipindi cha miaka 10 iliyopita, ongezeko la kila mwaka la idadi ya magari yaliyosajiliwa katika jiji ilikuwa asilimia 14, ikizidi ongezeko la idadi ya watu maradufu.

Kutokana na hali hiyo, msongamano wa magari kwenye barabara kuu umekuwa ukiongezeka kila mwaka na hivyo kukwamisha shughuli za kiuchumi.

Wasiwasi mkubwa ni kwamba kutokana na kasi ya ongezeko la watu katika jiji hivi sasa la asilimia 4, msongamano wa magari unatarajiwa kuongezeka zaidi katika siku zijazo.

Timu ya Maandalizi ya Utafiti ya JICA ilifika Tanzania Aprili 6 hadi Mei 12, 2014 kufanya utafiti huo na kuthibitisha kiwango cha uhitaji na uharaka wa uboreshaji wa barabara mpya ya Bagamoyo.

*Kiwango cha msaada wa Japan chini ya JICA kwa Tanzania kupitia mpango wa ushirikiano (Shilingi Milioni*)*

| | Msaada | Ushirikiano wa kiufundi | Mkopo |
|---|---|---|---|
| 2016 | 57,789 | 71,452 | 126,315 |
| 2017 | 5,410 | 47,831 | 0 |
| 2018 | 19,747 | 52,378 | 0 |
| 2019 | 39,473 | 45,620 | 0 |
| 2020 | 23,810 | 25,768 | 0 |
| Cumulative Total (1960 – 2020) | 2,710,080 | 2,047,747 | 1,688,842 |

*(*) Kiwango cha riba kilichotumika JPY= Sh21.0526 ( Chanzo Jica)*

Ushirikiano wa JICA katika Maendeleo ya Usafiri wa Mijini

Mwaka Jina la Mradi

1980 – 1982

**Mradi wa Upanuzi wa Daraja la Selander**

***1984 – 1987***
Mradi wa Uboreshaji wa Barabara ya Morogoro Awamu ya 1 & 2

***1992 – 1997***
Mradi wa Matengenezo ya Barabara ya Dar es Salaam Awamu ya 1 – 4

***1997 – 1999***
Mradi wa Uboreshaji wa Madaraja kwenye Barabara kuu, Awamu ya 1 & 2

***1997 – 2001***
Mradi wa Uboreshaji wa Barabara za Dar es Salaam Awamu ya 1 – 3

***2007 – 2009***
Mradi wa Upanuzi wa Barabara ya Kilwa

***2007 – 2008***
Sera ya Usafiri wa Dar es Salaam na Mpango Mkuu wa Maendeleo ya Mfumo

***2010 – 2014***
Mradi wa Upanuzi wa Barabara Mpya ya Bagamoyo Awamu ya 1

***2015 – 2018***
Mradi wa Uboreshaji wa Makutano ya Tazara (Daraja la juu la Mfugale )

***2010 – 2012***
Mradi wa Kujenga Uwezo wa Uboreshaji wa Usafiri wa Dar es Salaam

***2014 – 2017***
Mradi wa Kukuza Uwezo wa Uboreshaji wa Usafiri wa Dar es Salaam Awamu ya 2

***2016 – 2018***
Mradi wa Marekebisho ya Mpango Kabambe wa Usafiri wa Jiji la Dar es Salaam

***2019 – 2021***
Mradi wa Upanuzi wa Barabara Mpya ya Bagamoyo Awamu ya 2

***2019***
Present Mradi wa Uboreshaji wa Uwezo wa Usafiri jijini Dar es Salaam

## Mradi wa Upanuzi wa Barabara ya Mpya ya Bagamoyo

Mradi huo ulianzishwa ukiwa na njia nne na upana wa mita 9 kutoka katikati kwa ajili ya Usafiri wa Mabasi Yaendayo Haraka (BRT) katika eneo lenye takriban kilomita 4.3 kutoka katika mpaka wa miundombinu ya BRT ya awamu ya kwanza kwenye makutano ya barabara ya Morocco hadi Mwenge.

Babarabara za pembeni na maeneo ya watembea kwa miguu yalitengwa kwa ajili ya usalama na huduma za matengenezo ya magari ya baadaye.

Mifereji ya maji ya barabara kwa ajili ya kukabili mafuriko, vifaa vya usaidizi kwa kazi za barabarani na vifaa vya usalama barabarani viliwekwa pia.

TANGAZO

# UIMARISHAJI WA USHIRIKIANO BAINA YA TANZANIA NA JAPAN



Picha za muonekano wa baadaye wa Kituo kikuu cha Bandari ya Kigoma.



Daraja la juu la Mfugale.

Wanufaika wakuu wa mradi ni wakazi wa Dar es Salaam na wageni wa ndani na nje ya nchi.

Mradi huo ulilenga kuimarisha viwango vya vipato, kiuchumi, kuimarisha mtandao wa usafiri wa barabara kuu, kuboresha mazingira ya wakazi na kuondoa vikwazo vya uboreshaji uchumi na mtindo wa maisha wa wananchi katika eneo hilo lengwa la barabara.

Cha kushukuru ni kwamba inapunguza mafuriko barabarani, kupunguza msongamano, kuboresha udongo usiofaa ili kuzuia uharibifu wa uso wa lami na kuimarisha usalama barabarani.

Barabara ya New Bagamoyo huenda ikachangia kupunguza umaskini, ambalo ni lengo la pamoja katika mipango ya maendeleo ya taifa nchini Tanzania, na itasaidia kuboresha na kuimarisha mtandao wa barabara kuu.

Barabara mpya ya Bagamoyo iliyopanuliwa hailazimiki kutumia teknolojia ya hali ya kuifanyia matengenezo.

Mradi huo ulizingatia miongozo yote ya mazingira na kijamii.

Inaokoa muda wa kusafiri na gharama za usafirishaji. Pia uwezo wa barabara umeongezeka, hivyo kusababisha kuimarika kwa kiwango cha ufanisi wa usafiri jijini Dar es Salaam.

Barabara hiyo mpya inahakikisha uwepo wa abiria na usambazaji wa mizigo, kufika katikati ya jiji la Dar es Salaam kwa urahisi na vifaa vya bandari vitaboreshwa hivi karibuni, ambavyo kwa pamoja vitachangia ukuaji wa kijamii na kiuchumi.

Barabara hiyo iliyoboreshwa inatenganisha magari yanayosafiri kwa kasi ya kawaida dhidi ya yale yanayokwenda taratibu, kuhakikisha usalama na mtiririko mzuri wa magari.

Kupitia uimarishaji wa upatikanaji wa soko kutoka maeneo ya mashambani (Bunju na Bagamoyo) hadi sokoni, usafirishaji wa bidhaa umeimarika, hivyo basi kupunguza gharama za usafirishaji na kuchangia bei kuwa nafuu.

Vilevile, kasi ya wastani ya usafiri katika nyakati zinazokuwa na abiria wengi za asubuhi na jioni (Wastani wa masaa saba: kuanzia saa 12 hadi saa 4 asubuhi na kuanzia saa 10 hadi 1 jioni) imeongezeka kutoka km 3 kwa saa ( kutokana na msongamano) kufikia takriban km 40 kwa saa na hivyo kufupisha muda wa usafiri.

Uwezo wa usafirishaji wa magari umeongezeka kutoka magari 830 kwa saa na njia moja hadi magari 1,740 kwa saa na njia moja. Siku za barabara kufurika zinatarajiwa kupungua kutoka siku 30 kwa mwaka hadi siku 0 kwa mwaka.

Barabara ya Mpya ya Bagamoyo iliyopanuliwa inakidhi vigezo vya usanifu wa barabara kuu za hapa nchini. Barabara hiyo ilipangwa kutoshea tu ndani ya mtandao wa barabara kuu ikiwa ni pamoja na sehemu nyingine.

Mpango huo ulitathminiwa ili kuona kama unafaa katika taratibu za njia; njia iliyokuwapo ilifuatiliwa, lami na miundo iliyopo ilitumika kadri inavyowezekana, na athari hasi kwa mazingira ya kijamii zilipunguzwa.

Barabara hiyo ilijengwa katika namna ambayo itadumu kwa muda mrefu kwa kufanya matengenezo mepesi.

Viwango vya Kawaida vya Ujenzi wa Barabara vya mwaka 2000 vilitumika.

Pia, “Kiwango cha Usanifu wa Barabara nchini Japani - Maoni na Matumizi” na viwango vya kimataifa kama vile Kiwango cha Uingereza (BS) vilirejelewa kama inavyotakiwa.

Usanifu huo uliamua kujenga kwa ukubwa wa mita 4 hadi 6 barabara za pembeni kwa ajili ya kuhakikisha mtiririko mzuri wa magari huku ukizingatia mifumo iliyopitishwa katika Vituo vya Mabasi vya Makumbusho na Mwenge.

Njia za watembea kwa miguu zimejengwa kando ya barabara ili kuimarisha usalama kwa watembea kwa miguu.

Njia za mabasi zimeboreshwa na kujengwa ili kupunguza uwezekano wa ajali na kupunguza msongamano.

Taa za barabarani zimewekwa kando ya barabara ya Bagamoyo ili kuhudumia madereva na watembea kwa miguu kwa kuzingatia usalama wa magari usiku.

Upana wa kati wa barabara hiyo ni mita 9 ambayo itatumika kama njia ya BRT katika siku zijazo.

Kwa kuwa mradi huu ulitekelezwa chini ya msaada wa serikali ya Japani, njia ya utekelezaji na muundo wa ujenzi ulizingatia hali zote za kama vile hali ya hewa, ardhi, vitu vilivyomo nchini na changamoto ya msongamano.

Pia ilizingatia uwezo wa matengenezo ya ndani, utumiaji wa mbinu za utekelezaji za kawaida ambazo hazihitaji mashine maalumu za ujenzi au teknolojia, kuzingatia mazingira ya kijamii na usalama barabarani, na utumiaji na nyenzo zinazoweza kununuliwa ndani ya nchi kadri iwezekanavyo ili kuchangia katika uimarishaji wa uchumi wa nchi.

Mkandarasi wa mradi alizingatia taratibu za kazi kwa mujibu wa sheria zilizopo za ujenzi nchini, na alijitahidi kuzuia migogoro na wafanyakazi na kufanikiwa kufanya kazi katika mazingira salama zaidi. Mkandarasi alikuwa mwajiri wa fursa sawa.

Mkandarasi alizingatia masuala ya kijamii na kimazingira katika kipindi cha kazi.

Njia za ujenzi zilizotumika zililenga kupunguza vumbi na vipande vidogo vidogo. Mimea ambayo husababisha kelele na vipande vidogo vidogo viliondolewa mbali na makazi ya watu.

Taka zinazozalishwa zilisafirishwa hadi kwenye maeneo mahususi kwa utupaji wa taka. Maji machafu yaliyotoka katika mimea yalitibiwa ipasavyo kulingana na taratibu za Kitanzania.

Usalama wakati wa kazi ulizingatiwa, vifaa vya usalama kama vile vizuizi, koni za rangi, taa zinazozunguka zilitumiwa. Pia vidhibiti usalama barabarani viliwekwa.

**Ushirikiano zaidi wa Japan na Tanzania**

JICA pamoja na Serikali ilipendekeza dhana ya “Maendeleo yaliyojikita katika kukuza usafiri.”

Dhana hii inahimiza kutoka katika mfumo wa matumizi ya usafiri binafsi hadi matumizi ya usafiri wa umma.

Kuongeza uwezo wa barabara kukidhi mahitaji yanayoongezeka ni ngumu, kwa hivyo mabadiliko ya mifumo yanaweza kuboreshwa.

Sio tu ukuzaji wa sehemu za usafiri kama vile kituo cha MRT/BRT, lakini pia kuimarisha mvuto wa maeneo karibu na usafiri wa umma katika kituo kidogo, kituo cha Wilaya na/au Jiji.

JICA inadhani kuwa dhana hiyo itachangia mapato ya ziada kwa usafiri wa umma (kama vile BRT) ili waweze kuwekeza tena katika awamu iliyobaki ya miradi.

Zaidi ya hayo, JICA inafikiria kutanua wigo wa ushirikiano wake kwa mji mkuu wa Dodoma.

Pamoja na mpango madhubuti na uongozi wa Serikali ya Tanzania, mji mkuu unakua kwa kasi zaidi. Ili kukabiliana na ongezeko la mahitaji ya usalama barabarani, JICA inafanya upembuzi yakinifu wa maendeleo ya barabara za ndani ya jiji.

JICA pia itaendeleza ushirikiano wake katika maendeleo ya ukanda. Miradi ambayo ipo katika hatua ya mipango ni “Mradi wa Ukarabati wa Bandari ya Kigoma” na “Mradi wa Uboreshaji wa Barabara ya Arusha-Holili.”

Miradi hii itashughulikia masuala ya usalama pamoja na uboreshaji wa ufanisi wa usafirishaji wa kanda za kiuchumi.

Bandari ya Kigoma ni kitovu cha usafirishaji cha Ukanda wa Kati unaounganisha Tanzania, Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo kupitia Ziwa Tanganyika.

Wakati usafiri wa ziwani ukiwa ni njia muhimu kwa wakazi wa eneo hilo, kituo cha abiria kimepata hitilafu kubwa, na watu hawawezi kupanda katika chombo hiko moja kwa moja.

Barabara ya Arusha-Holili ni njia kuu ya usafiri kati ya Arusha na Kenya. Mradi ujao utaongeza uwezo wa barabara kupitisha magari kwa kupanua sehemu zenye shughuli nyingi.

Aidha, mradi utaondoa msongamano katika sehemu ya daraja la Kikafu kati ya Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro na Moshi.

Mwisho kabisa, wakati wa utengenezaji wa miundombinu ya usafiri, ni muhimu kuwa na msaada wa namna bora ya utumiaji wa miundombinu iliyoanzishwa.

Kwa ajili ya maendeleo na matumizi bora ya miundombinu, JICA imekuwa ikijishughulisha na maendeleo ya rasilimali watu husika.

Program ya Uundaji Ushirikiano wa Maarifa wa JICA (KCCP) inawaalika Watanzania nchini Japan, na inahusiana na matumizi ya uzoefu wa maendeleo ya Japan na ujuzi kwa kurekebisha uendane na nchi mshirika, badala kutegemea usambazaji wa teknolojia na ujuzi wa hali ya juu wa Japan pekee.

Tangu kuanza kwa ushirikiano huo, zaidi ya Watanzania 21,000 walitembelea Japan kwa ajili ya mafunzo. JICA itaendelea kuendesha program ya KCCP kwa maendeleo zaidi ya rasilimali watu katika sekta ya uchukuzi na sekta nyingine zinazohusiana.

JICA, kupitia miradi inayokuja hivi karibuni, itachangia katika maendeleo zaidi ya Tanzania bega kwa bega na wananchi na Serikali ya Tanzania, na kuimarisha ushirikiano wa muda mrefu kati ya Tanzania na Japan.



Muonekano wa daraja la Selander mwaka 1982



Majaribio ya ukaguzi usio na madhara wa matofali huko Japan.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Maandalizi makubwa yanahitajika kwa Tembo Warriors Kombe la Dunia

**TIMU** ya Taifa ya Tanzania ya Soka kwa Watu wenye Ulemavu wa viungo 'Tembo Warriors', imeweka rekodi nchini kwa kuwa timu ya kwanza kufuzu fainali za Kombe la Dunia kwa upande wa mpira wa miguu.

Tembo Warriors imeweka rekodi hiyo wiki iliyopita baada ya kufanikiwa kutinga nusu fainali ya Fainali za Maraifa Afrika kwa watu wenye Ulemavu (CANAF), zilizomalizika hapa nchini kwa Ghana kutwaa ubingwa baada ya kuwachapa mabingwa wa zamani wa dunia, Angola kwa mabao 3-2.

Katika fainali hizo za CANAF, timu nne zilizotinga nusu fainali; Angola, Liberia, Ghana na Tanzania, zimefuzu moja kwa moja kushiriki fainali za Kombe la Dunia zitakazofanyika mwakani nchini Uturuki.

Hata hivyo, Tembo Warriors ilimaliza katika nafasi ya nne baada ya kutolewa na Liberia hatua ya nusu fainali na kisha kukubali kichapo cha mabao 4-0 kwenye mechi ya kutafuta mshindi wa tatu dhidi ya Liberia.

Lakini juhudi na malengo makubwa kwa Tembo Warriors ilikuwa kufuzu kwanza fainali hizo, lengo ambalo limetimia na sasa inachotakiwa ni kufanya maandalizi makubwa kuelekea Uturuki mwakani.

Kwanza kabisa kwa hatua iliyofikia Tembo Warriors, hatuna budi kuipongeza na kuwa kitu kimoja katika kuiunga mkono kwa hali na mali ili mwakani kuweza kuipeperusha vema bendera ya nchi kimataifa.

Kwa juhudi zilizoonyeshwa na kila mchezaji ikiwa ni pamoja na kucheza kitimu, kuna haja ya mashabiki, wadau wa soka, serikali na Watanzania kwa ujumla kila mmoja kwa nafasi yake kutupia jicho timu hii kwa kuisaidia ili kwenda kufanya vizuri.

Kwa namna ilivyocheza michuano ya CANAF, ni wazi katika Kombe la Dunia itakutana na timu nzuri na ngumu zaidi, hivyo maandalizi makubwa yanahitajika kuanzia sasa ili kuweza kwenda kufanya makubwa zaidi katika fainali hizo mwakani nchini Uturuki.

Tunaelewa kwa sasa inahitaji kutafutiwa mazingira mazuri iwe ndani ama nje ya nchi kwenda kuweka kambi kwa ajili ya kujiandaa na fainali hizo za Kombe la Dunia kwa kupata mechi nyingi za kirafiki.

Maandalizi hayo yanahitaji fedha nyingi ili kuweza kukidhi gharama mbalimbali, jambo ambalo linahitaji kuungana mkono kwa pamoja ili kuiwezesha kwenda kuipeperusha vema bendera ya nchi kimataifa.

Hii ni kutokana na ukweli kwamba, baadhi ya wachezaji wanaounda kikosi cha Tembo Warriors wapo wenye familia na soka wanalocheza haliwaingizii kipato kikubwa kwa sasa kutokana na kutokuwa na wadhamini, hivyo wanahitaji kuziacha familia zao katika mazingira mazuri ili kuweza kuelekeza akili zao mchezoni.

Pamoja na hayo yote, lakini huu ni wakati sasa kwa wadhamini mbalimbali kujitokeza kuidhamini Tembo Warriors sambamba na kumulikwa ustawi mzima wa soka la wenye ulemavu nchini ili kuwa na timu ya taifa imara zaidi.

Nipashe tunatamani kuona sasa kukianzishwa klabu nyingi za soka za watu wenye ulemavu na ligi yao ikipata wadhamini wengi ili kutoa ushindani kwani tayari wamedhihirisha wanaweza kuiletea sifa kubwa nchi katika anga ya michezo.

Aidha, mawakala hawana budi sasa kugeukia soka la watu wenye ulemavu kwa kuanza kuwatafutia klabu kubwa nje ya nchi ili kwenda kucheza soka la ushindani zaidi kwa manufaa yao binafsi na timu ya taifa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Kamera za televisheni ziongezwe Ligi Kuu

Na Adam Fungamwango

**HADI** kufikia raundi ya saba ya Ligi Kuu, kumekuwa na maamuzi yenye utata mkubwa kwa marefa wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu.

Tumeona jinsi waamuzi wanavyovurunda kwenye baadhi ya maamuzi yao na kuwaacha mashabiki wa soka na wachambuzi kwenye maswali mengi yasiyojibika.

Haieleweki kama ni uwezo mdogo wa marefa, makusudi, mapenzi au pengine rushwa ndiyo inayosababisha marefa wafanye baadhi ya maamuzi yanayoziumiza timu nyingine.

Tumeshuhudia mabao yenye utata, au ambayo yamekataliwa kwa sababu zisizoeleweka. Kuna kadi zimetoka ambazo hazikutakiwa zitoke, au hazikuwa na ulazima, pia kuna mikwaju ya penalti imetolewa na waamuzi au kukataliwa kiutata.

Hata hivyo, kuna baadhi ya matukio ambayo yanaonyesha kuwa marefa walitoa maamuzi sahihi, lakini wakahukumiwa na baadhi ya wachambuzi wa soka na mashabiki kutokana na uchache wa kamera zinazoonyesha mechi hizo.

Mfano ni mechi ya Jumatano iliyopigwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Simba ikishinda mabao 2-1. Moja ya tukio ni kukataliwa kwa bao la pili na la kusawazisha la Geita Gold. Shomari Kapombe alionekana kuruka na kuukosa mpira, mshambuliaji George Pole akapiga kichwa mpira ukajaa wavuni.

Kila mmoja aliyeangalia kwenye televisheni na baadhi ya waliokuwa uwanjani, walishangaa ni kwa nini mwamuzi Martin Saanya alilikataa bao lile, lakini pia wapo waliotafsiri kuwa alikuwa sahihi kwa kuwa kabla ya kuruka alimchezea madhambi Kapombe na mwamuzi alipuliza kipenga hata kabla hajaupiga mpira kwa kichwa.

Marudio ya televisheni, yalionyesha alimgusa kidogo, lakini baada ya kureja kutazama sana. Hiyo yote ikitokana na uhaba wa kamera iliyowekwa laivu ikiwaonyesha Mpole na Kapombe kabla mpira haujapigwa na wakati umewafikia. Kilichokuwa kikionekana ni mpira ukiwa juu unakuja golini. Halafu ghafla anaonekana Kapombe yupo juu akionekana kama amesukumwa na papo papo Mpole akaruka na kuupiga kichwa mpira ukajaa wavuni.

Tukio hili lilileta mjadala mkali sana kwenye vipindi vya michezo redioni, televisheni, na hata kwenye mitandao ya kijamii. Watangazaji na wachambuzi, walimkalia kooni mwamuzi Saanya kuwa alivurunda kwa kuwakataliwa Geita Gold bao lao halali.

Kesho yake kiliibuka kipande cha video, sijui kilitoka wapi, au kilifichwa wapi, kinachoonyesha Mpole akiwa anamsukuma Kapombe alipokuwa anataka kuruka, akakosa balansi, pamoja na kuruka, lakini akaukosa mpira akaanguka. Mpole akaruka na kufunga.

Kipande hiki ambacho hakikuonekana siku mechi ilipokuwa inaonyeshwa laivu, kikabadilisha msimamo wa watangazaji, wachambuzi na baadhi ya mashabiki kuwa ni kweli halikuwa bao halali na mwamuzi Saanya alikuwa sahihi. Baadhi wakaomba radhi.

Nadhani kipande hiki kingeonyeshwa mechi ilipokuwa inachezwa laivu mjadala ule mkali usingekuwapo. Kila aliyeangalia angejua ni kweli Kapombe amesukumwa.

Dunia ya sasa ni ya teknolojia, tofauti na zamani ambapo watu walikuwa wanasikiliza kwenye redio, hivyo hata kama bao lina utata, au limekataliwa bao halali kulikuwa hakuna mijadala kwa sababu mashabiki hawaoni bali wanasikiliza tu.

Lakini kwa sasa mijadala huwa inazuka na mashinikizo kwa waamuzi, wachezaji wanazidi kwa sababu watu wanaangalia laivu kila kitu kinachofanyika kwenye televisheni.

Tatizo linakuja pale televisheni inayoonyesha inaonekana kama kuruka baadhi ya vipande, au kuwa na kamera chache ambazo zinashindwa kulionyesha tukio hilo kwa usahihi zaidi.

Hii inazidi kuleta tafrani na mijadala, kwa sababu kila mmoja anakuwa anatafsiri kivyake kwa jinsi anavyotaka yeye.

Kwa maana hiyo, Kampuni ya Azam Media, ambayo ina haki ya kuonyesha mechi hizo za Ligi Kuu, sasa iongeze kamera zake ili kuondoa utata kwenye matukio kama hayo.

Kuna matukio ambayo wala huhitaji kamera za upande fulani kujua kitu gani kimefanyika, lakini kuna matukio ambayo yanahitaji kamera kwenye 'engo' ili kuthibitisha.

Watu hawataki kamera ziongezwe ili wajue kama limetokea, limefanyika, ili matokeo yafutwe la hasha, kwa sababu hata kama mwamuzi amekosea, lakini maamuzi yake ni ya mwisho 'akisema ni makosa basi ni makosa', ila wanachotaka ni kuona kama tukio ni sahihi au siyo, ili wakati mwingine kuepusha mijadala isiyo na tija kwenye mitandao ya kijamii.

Mfano mechi ya Simba na Geita Gold, wachambuzi walitumia muda karibu wote wa vipindi kuzungumzia bao lililokataliwa kuliko umahiri wa kusakata kandanda waliouonyesha Geita Gold.

HABARI KITAIFA

# Makalla: Miradi mikubwa Kinondoni kuanza kwa kasi

**Na Jenifer Gilla**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, amesema miradi mikubwa mitatu katika Wilaya ya Kinondoni ukiwamo wa Stendi ya Mwenge, itaanza kutekelezwa kwa kasi baada ya maadhimisho ya miaka 60 ya Uhuru.

Aliyasema hayo katika sherehe za uzinduzi wa barabara ya Mwenge-Morocco yenye urefu wa kilomita 4.3, katika viwanja ya Chuo cha Ustawi wa Jamii, jijini Dar es Salaam jana, wakati akimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuidhinisha fedha za kujenga miradi hiyo.

Aliitaja miradi hiyo kuwa ni uwanja mkubwa wa mpira utakaogharimu Shilingi bilioni nne, stendi ya mabasi ya kisasa ya Mwenge na ujenzi wa jengo la utawala la Manispaa ya Kinondoni.

"Katikati palitokea dosari, na mheshimiwa Waziri Mwalimu (Ummy) alikuja, akaziona hizo dosari na tukazifanyia kazi, ameshatoa maelekezo kwangu kuwa baada ya kamati yangu kurekebisha zile dosari zilizojitokeza, ameidhinisha ujenzi sasa uendelee, na mimi nikuhakikishie wiki ijayo baada ya Uhuru, majengo yale na miradi yote mitatu itajengwa kwa kasi kwa sababu fedha zipo katika Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni," alisema Makalla.

Juni 20, mwaka huu, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ummy Mwalimu alimsimamisha kazi mhandisi Isack Mpaki anayesimamia miradi hiyo baada ya kutoridhishwa na mwenendo wa ujenzi wa mradi huo.

Waziri Ummy alifikia uamuzi huo baada ya kutembelea na kukagua miradi na kusema tangu ulipoanza hadi alipoutembelea ulifikia asilimia 46 ya utekelezaji, licha ya kuongezewa muda.

Makalla alimshukuru Rais Samia kwa kuidhinisha Sh. bilioni 165 zitakazotumika kutekeleza mradi mkubwa wa maji katika Jimbo la Kawe na kutatua kero ya maji.

" Umefanya jambo kubwa sana kwa Jimbo la Kawe kuidhinisha fedha Sh. bilioni 165 kwa ajili ya mradi wa maji ambao utanufaisha watu wa Makongo, Wazo, Bunju Boko, Goba, Mabwepande, Mbweni, na kwa sababu ni mradi mkubwa tutakualika uje uutembelee," alisema.

Alisema pia mgawo wa maji unaelekea ukingoni kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha.

"Na kwasababu nimeongelea habari ya maji basi niwahakikishie tuliomba mvua inyeshe na imenyesha, sasa maji yemerejea na tuendelee kuomba kwamba mvua zikiendelea kunyesha basi mgawo hautokuwapo tena," alisema Makalla.

# Serikali yatoa tamko Mtanzania kukutwa kirusi kipya

**Na Christina Mwakangale**

SERIKALI imetoa ufafanuzi kuhusu kuwapo kwa taarifa za Mtanzania kupatikana na aina mpya ya kirusi cha corona kiitwacho Omicron, ikisema haijabainika iwapo mtu huyo alipatia maambukizi hapa nchini au la.

Pia imesema Maabara Kuu ya Taifa, imeendelea kusimamia upimaji wa ugonjwa wa Uviko-19 pamoja na kuangalia anuwai mpya zinazosababishwa na mabadiliko ya mara kwa mara ikiwamo kirusi cha Omicron.

Katibu Mkuu Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Prof. Abel Makubi, aliyasema hayo jana mkoani Dar es Salaam, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu taarifa hizo ambazo zilisambaa nchini kupitia mitandao ya jamii na kuanza kuleta hofu miongoni mwa wananchi.

"Hivi karibuni kumetokea unuwai mpya ijulikanayo kama Omicron (B.1.1.529) iliyoripotiwa kwa mara ya kwanza Afrika ya Kusini na Botswana. Leo (jana), tumepokea taarifa iliyoripotiwa na vyombo vya habari vya India na kuenea katika mitandao ya kijamii na kueleza kuwa India wamegundua abiria mmoja anayerudi nyumbani (India) mwenye anuwai mpya Omicron, ametokea Tanzania.

"Hata hivyo haijajulikana kama abiria huyu alitokea Tanzania moja kwa moja au alipita Tanzania kuelekea India. Pia haijulikani alipita wapi kabla ya kufika India. Kutokana na taarifa hizo, Wizara ya Afya, imeanza kufuatilia kupitia vyombo vyetu vya ndani kwa kushirikiana na ubalozi wa Tanzania nchini India, ili kubaini ukweli wa jambo hili na baadaye kuchukua hatua stahili," alisema Prof. Makubi.

Alibainisha kwamba, wananchi waondoe hofu kutokana na habari hizo, bali kuendelea kuwa watulivu na kufanya shughuli za maendeleo kama kawaida, huku wakichukua tahadhari zote, kwa kunawa mikono kwa sabuni na maji tiririka, kuvaa barakoa na kujiepusha na misongamano isiyokuwa ya lazima na kufuata miongozo ya wizara kuhusu kupambana na Uviko-19.

Prof. Makubi alisema, wizara inachukua hatua zaidi za kuepusha nchi isiingie kwenye mlipuko wa nne kwa kufanya upimaji kwenye mipaka na viwanja vya ndege kwa watu wote wanaosafiri kwenda nje ya nchi.

"Wasafiri wanaogundulika hawana maambukizi ya Uviko-19 kwa kutumia kipimo cha RT-PCR hupewa cheti kuwaruhusu kusafiri. Wasafiri wanaogundulika kuwa na maambukizi huunganishwa na daktari/hospitali, ili waanze matibabu na kuwa katika uangalizi maalumu na kufuatiliwa kupitia mawasiliano yake. "Maabara ya taifa pia imekuwa ikichunguza mabadiliko ya kirusi, kuangalia uwapo wa anuwai mbalimbali zinazotokana na mabadiliko mapya ya Omicron. Tunaomba kuwatoa wasiwasi Watanzania wote mpaka sasa hatujabaini anuwai mpya, Omicron," alisema Prof. Makubi.

Aidha, Prof Makubi, aliagiza viogozi wote wa mikoa na wilaya, kuweka na kukagua miundombinu hasa sabuni na maji ya kunawa mikono sehemu za mikusanyiko ili kujikinga, bila kusubiri athari kubwa.

"Tunawahimiza wananchi kujitokeza kuchanja ili kujikinga na UVIKO-19 na kuanzia Desemba 7, mwaka huu, tutakuwa na kampeni maalumu za elimu za kuhamasisha wananchi wengi zaidi wajitokeze kuchanja katika kuadhimisha miaka 60 ya Uhuru wa nchi yetu.

"Kampeni hizo zitafanyika katika ngazi za mitaa, masoko, viwanja vya mipira, stendi za basi/daladala, vyuo na kwenye taasisi mbalimbali. Nawaomba viongozi wote katika mikoa, wilaya, mitaa na vijiji, tusimamie zoezi hili kwa ufanisi," alisema.


EAST AFRICAN
CRUDE OIL
PIPELINE

**OMBI LA KUONESHA NIA YA UTENGENEZAJI NA USAMBAZAJI WA DOHANI ZA JIKONI**
**KUMBUKUMBU: 0010007327**

Kampuni ya Kimataifa ya Mafuta na Gesi ya TotalEnergies East Africa Midstream B.V, inaalika taasisi zenye weledi na uzoefu kuonesha nia ya kutoa huduma ya utengenezaji na usambazaji wa Dohani za Jikoni katika Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP).

Mradi wa EACOP unahusisha ujenzi na uendeshaji wa bomba litakalofukiwa chini ya ardhi litakalovuka mipaka ya nchi mbili na litakalosafirisha mafuta kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka Pwani ya Mashariki ya Tanzania kwa ajili ya kusafirisha mafuta hayo kwenda katika masoko ya Kimataifa. Bomba hili litaanzia Kabaale katika wilaya ya Hoima nchini Uganda, mpaka Chongoleani, Mkoani Tanga nchini Tanzania. Urefu wa Bomba ni kilomita 1,443, kati ya hizo, kilomita 1,147 zitakuwa Tanzania, ambapo bomba hilo litapita kwenye mikoa minane (8) ambayo ni Kagera, Geita, Shinyanga, Tabora, Singida, Dodoma, Manyara, na Tanga; bomba la mafuta pia litapita kwenye Halmashauri za Wilaya 27 na vijiji 231.

**MAELEZO MAFUPI KUHUSU MAWANDA YA HUDUMA:**
EACOP inahitaji huduma za mtengenezaji mwenye uzoefu na mwenye sifa nzuri kutoa huduma za Utengenezaji na Usamabazaji wa Dohani za Majiko na kitolea mvuko wake kulingana na viwango, vipimo na maelezo yaliyotajwa hapa chini:

**VIWANGO:**
Nyenzo, uzalishaji na uunganishaji wa Dohani za Majiko utazingatia viwango vya BS: 1449: Part 2: 1983 – vyuma vinavyoweza kuhilimi joto, pamoja na marekebisho yake ya hivi karibuni, isipokuwa kama itabainishwa vinginevyo.

**MAELEZO YA JUMLA YA DOHANI:**
- Dohani lazima liwe la ukubwa wa 250mm kwa 250mm. Liwe la urefu wa 1.5m. liwe limefungwa na chuma za 32mm kwa kutumia bolt za unene wa 10mm.
- Mdomo wa Dohani (kitolea mvuke) lazima uwe na ukubwa wa 950mm kwa 600mm kwa 500mm na kufungwa na chuma za 25mm itakayochomelewa katika pande zote za Dohani.

**VIGEZO MUHIMU:**
- MSAMBAZAJI atakuwa na uwezo wa kiwango cha chini cha usambazaji wa Dohani 30, vitolea mvuke na vifaa vyake kwa mwezi ili kukidhi kiwango kitakachohitajika na KAMPUNI. KAMPUNI inategemea kuwa na uhitaji wa angalau Dohani 220 na vifaa vyake kwa jumla, kwa kiwango kilichoainishwa hapo juu cha Dohani 30 na vifaa vyake kwa mwezi.
- Hakuna nyenzo au viambatisho vitatumika katika utengenezaji hadi kibali cha awali cha matumizi yake kitolewe na KAMPUNI; wala mabadiliko yoyote katika asili, ubora, aina, na chanzo cha usambazaji hakitafanywa bila ruhusa ya KAMPUNI.
- Kwa ombi, nyaraka za ubora wa bidhaa zinazotolewa zinapaswa kuwasilishwa na mtengenezaji kupitia vyeti vya kufanya kazi kulingana na viwango vinavyotumika. Rekodi zote za matokeo ya vipimo vya ubora zitahifadhiwa na mtengenezaji kwa marejesho yajayo.
- Kabla na baada ya kutoa zabuni kwa Mtengenezaji, KAMPUNI ina haki ya kukagua uwezo wa upimaji na kushuhudia majaribio yaliyofanywa katika kituo cha Maabara cha Mtengenezaji kutathmini ubora wa bidhaa kulingana na viwango vinavyotumika.
- KAMPUNI itateua mwakilishi kushuhudia majaribio yote yaliyofanywa katika kituo cha maabara cha Mtengenezaji na mwakilishi atawasilisha matokeo yote ya mkandarasi/mzabuni husika & KAMPUNI kwa kujitegemea. KAMPUNI ina haki ya kuidhinisha Bidhaa kulingana na ripoti za majaribio ya ubora kabla ya kupelekwa kwenye eneo la ujenzi.
- Dohani ya Jikoni na maunzi yake yote yatakuja na dhamana ya vifaa na utengenezaji kwa muda wa miezi 12 tangu tarehe ya kukabidhi.

**VIGEZO MUHIMU VYA KUZINGATIA:**
Taasisi zitakazoonesha nia zinaalikwa kuambatanisha maombi yao pamoja na taarifa zifuatazo:
- Uzoefu, utendaji, na uwezo katika kutekeleza kazi zilizoainishwa chini ya upeo wa kazi, kwa kiwango kikubwa nchini Tanzania, kwa kufuata viwango vya kitaifa na kimataifa (ikiwa ni pamoja na Viwango vya Shirika la Fedha la Kimataifa (IFC), na uzoefu wa angalau miaka 10 katika utendaji wa huduma kama hizo ndani ya Tanzania au Kimataifa.
- Uthibitisho wa usajili wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) pamoja na cheti cha uthibitisho wa kulipa kodi kwa mwaka wa fedha uliopita.

**Maelezo mafupi kuhusu uzoefu na uwezo wa:**
- Utekelezaji wa programu za aina hiyo kwa viwango vya fedha vya kimataifa kwa ajili ya miradi mikubwa ya miundombinu nchini Tanzania.
- Kusimamia miradi mikubwa na wakandarasi washirika.
- kufanya kazi kwa kushirikiana na serikali za mitaa na sekta binafsi.
- Wafanyakazi waliopendekezwa kufanya kazi kwenye Mradi huu na ujuzi na uzoefu wao katika kutekeleza programu za aina hii.
- Inashauriwa, muonesha nia atume maombi ya kusajiliwa na kanzi data ya EWURA (LSSP) kama mtoaji na msambazaji wa huduma ndani ya nchi wakati wa kuwasilisha ombi la kuonesha nia ya kutekeleza shughuli za progamu.
- Kuzingatia Kanuni za maudhui ya ndani, 2017 na ufafanuzi wa Kampuni ya Ndani

Mawanda haya yanaweza kugawanywa kimkoa au kiutalaam na KAMPUNI inaruhusu Wazabuni kuwasilisha pendekezo kwa ajili ya kipengele kimoja, kadhaa au vyote.

Taasisi zenye nia ya kuleta maombi na ambazo zina uwezo na rasilimali za kutekeleza shughuli au kazi zilizoorodheshwa hapo juu zinapaswa kueleza nia yao pamoja na kuambatanisha pamoja na nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia barua pepe kwa **eacop-tz.eoi.1000001@totalenergies.com** (ukubwa wa barua pepe 20 Mb) saa au kabla ya saa **11** Jioni Afrika Mashariki (EAT) tarehe **23rd, December 2021.** Kichwa cha Barua Pepe ni **0010007327.**

**Muhimu:** Mradi wa EACOP utapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na taasisi zitakazoonyesha nia ili kutengeneza orodha ya taasisi za awali zenye vigezo vinavyotakiwa. Taasisi zitakazokidhi vigezo tu ndiyo zitapokea na kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA) pamoja na mwaliko wa kuwasilisha zabuni katika kuendeleza mchakato wa zabuni. Maelezo yote ya kuonyesha nia yanapaswa kuandikwa kwa lugha ya Kiingereza.

216600602

# Aweso aagiza bei sawa maji mijini na vijijini

**Na Renatha Msungu,**

WAZIRI wa Maji, Juma Aweso, ameziagiza Mamlaka za Maji nchini kupanga bei sawa ya gharama za bili ya maji mijini na vijijini ili kuepuka kuwakandamiza wananchi wengine hususani wa vijijini.

Aliyasema hayo wakati wa uzinduzi wa kusukuma maji kwa kutumia umeme wa jua badala ya kutumia mafuta ya dizeli.

Mradi huo ambao umefadhiliwa na Benki ya Dunia kwa kushirikiana na Benki ya Biashara (TIB), una thamani ya Dola za Kimarekani Sh. milioni 700, na vijiji 127 vitanufaika na mradi huo katika mikoa ya Dodoma, Shinyanga, Singida, Tabora na Mtwara.

Alisema mamlaka nyingine zimekuwa zikipanga bei kubwa na katika Mkoa wa Dar es Salaam uniti moja inauzwa kwa Sh. 1,000, wakati sehemu za pembezoni huuziwa Sh. 2,500 mpaka 5,000.

"Naomba wote muwe na bei moja kwa sababu maji yote ni sawa sasa kwanini wengine wabebeshwe mzigo mzito tena walioko vijijini," alihoji Aweso.

Aliagiza kuanzia jana tabia hiyo ikome kwa kuwa wananchi wote ni sawa na wanahitaji kupata haki sawa katika huduma ya majisafi na salama.

Pia alimtaka mhandishi wa DUWASA kuhakikisha bei hizo zinabadilika mara moja ili zianze kutumika sawa sawa na sehemu nyingine.

Kadhalika, ameagiza katika kijiji cha Magulo, Ilindi na Mpamatwa kuhakikisha kunachimbwa visima ili wananchi waweze kupata majisafi na salama.

Alimtaka mhandishi kutumia fedha alizonazo katika akaunti kuchimba visima na kusisitiza kazi hiyo ianze mapema.

Naye Kaimu Mkurugenzi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), Mhandisi Mkama Bwire, alisema kutokana na mpango wananchi watalipa maji kulingana na matumizi yao ya kila siku.

Alisema iko wazi kwamba kila mwananchi aliyeko vijijini na mijini ana wajibu wa kupata mjisafi na salama kwa ajili ya matumizi mbalimbali kiafya.

Hata hivyo, alisema malengo makubwa ya kuanzishwa kwa RUWASA ni kuhakikisha wananchi wote wanapata huduma ya majisafi na salama na taasisi hiyo itaibua na kujenga miradi ya maji hususani katika maeneo ya pembezoni.

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya ya Bahi, Mwanahamisi Mkunda, alimshukuru Waziri Aweso kutokana na kuwapa huduma ya maji katika wilaya hiyo, huku akiomba RUWASA kufanya kazi kwa haraka kuhakikisha maji yanapatikana kwa wananchi.




Mshindi wa kwanza wa pikipiki katika kampeni ya Tigo ya mwisho wa mwaka inayoitwa 'Wagiftishe - Gift Juu ya Gift', Noel Kabuje, mkazi wa Kurasini, akionyesha furaha baada ya kukabidhiwa zawadi yake jijini Dar es Salaam jana, ambapo wateja wanatakiwa kununua ITEL T20 kwa bei ya 89,000/- kutoka duka lolote la Tigo nchini kote ili kupata nafasi ya kujishindia simu janja 504 na pikipiki 1 kila wiki kwa muda wa wiki 6. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Diwani matatani kukutwa na korosho chafu

**Na Said Hamdani,** LINDI

DIWANI wa Kata ya Tingi, Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa, mkoani Lindi, Rajabu Ngatanda (CCM), anashikiliwa na Polisi Wilaya ya Liwale kwa tuhuma za kukutwa na magunia zaidi ya 80 ya korosho chafu.

Kwa mujibu wa taarifa kutoka Liwale na kuthibitishwa na Kamanda wa Polisi mkoani humo, ACP Mtatiro Kitinkwi, Ngatanda alikamatwa Liwale Mjini, Desemba mosi mwaka huu, kufuatia raia wema kuibua njama hizo.

Alisema mtuhumiwa alikamatwa na idadi hiyo ya korosho zinazodaiwa ni chafu akiwa amezisafirisha katika lori lenye namba za usajili T213 DPP na tela T806 DPG likitoka Wilaya ya Kilwa kwenda Liwale.

Kitinkwi alisema kutokana na kitendo cha mtuhumiwa kutaka kuchafua sifa za korosho za Liwale, raia wema walitoa taarifa kwa jeshi hilo na askari walipofika eneo husika walimtia nguvuni na kumfikisha kituoni kwa mahojiano.

Vile vile, Kamanda alisema mtuhumiwa atafikishwa mahakamani kujibu shtaka linalomkabiri baada ya kukamilisha mahojiano na taratibu zingine.

Baadhi ya mashuhuda, ambao hawakutaka majina yao kuandikwa gazetini, wamedai diwani huyo amekuwa na tabia ya kupeleka korosho chafu kutoka Mkoa wa Pwani na Kilwa lengo likiwa ni kuchanganya na safi za Liwale.

"Diwani huyu anatumia cheo chake kujinufaisha na kutaka kuchafua sifa nzuri ya korosho zinazolimwa Liwale," alidai mmoja wa mashuhuda hao.

Walidai katika utaratibu huo, diwani huyo anadaiwa kushirikiana na baadhi ya watu wa Wilaya ya Liwale kuhujumu korosho zao ambazo zimekuwa na sifa za ubora ikilinganishwa na maeneo mengine.

# Mwekezaji mzalendo ahofu kupokwa hoteli

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

MWEKEZAJI mzalendo wa hoteli mjini hapa, Peter Sipano Meelta, amedai yupo hatarini kudhulumiwa hoteli yake na mwekezaji kutoka nchini Uturuki.

Akizungumza na waandishi wa habari, alisema ameamua kupeleka malalamiko kwa Mkuu wa Mkoa huo, Ayoub Mohamed Mahmoud, baada ya kubaini kuna mpango wa kubadilishwa mkataba wa ukodishwaji.

"Nilikodisha hoteli kwa Kampuni ya Zanfood Trading Limited ili waweze kuendesha, lakini sasa wamenigeuka wanasema hoteli mali yao wakati hawajawahi kujenga tofali hata moja au msumari," alilalamika.

Alisema baada ya kujitokeza tatizo hilo aliamua kuwasilikisha malalamiko kwa Mkuu wa Mkoa kabla ya kukamatwa na kuwekwa ndani kwa muda wa siku nne katika Kituo cha Polisi Kiwengwa kwa tuhuma za kutaka kuhatarisha usalama kwa wageni na uvunjifu wa amani.

Alisema Mkuu wa Mkoa baada ya kupokea malalamiko aliamua kuitisha kikao cha pamoja kati ya Peter Sipano Meelta na mwekezaji kutoka Uturuki, Erkan Acikel ili kusikiliza pande zote mbili na kuwataka kuendelea na mazungumzo ya kutafuta mwafaka.

"Kinachosikitisha mimi natetea mali yangu ndiyo nimekamatwa na kuwekwa mahabusu kwa muda wa siku nne kwa amri ya Mkuu wa Mkoa badala ya serikali kunisaidia kupata mali yangu," alidai. Aliiomba serikali kuunda kamati maalum ya kuchunguza mgogoro huo ili ukweli uweze kupatikana na kuhakikisha haki inatendeka baada ya kuanza kujitokeza upotoshaji tangu kuanza kwa sakata hilo.

Meelta alidai mwekezaji huyo sasa amezuia kupita katika eneo la wazi ndani ya hoteli wakati nyumba anayoishi imo ndani ya hoteli na kuwapa wakati mgumu yeye na familia yake. Alidai Alhamisi iliyopita usiku alinusurika kushambuliwa na visu na kulazimika kukimbilia nje ya hoteli jambo ambalo lilisababisha mkusanyiko wa watu.

Akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake Mkokotoni, Mkuu wa Mkoa Kaskazini Unguja, Ayoub Mohamed Mahmoud, alithibitisha kupokea malalamiko ya mgogoro kutoka kwa mwekezaji wa kizalendo na kulazimika kuwakutanisha.

"Kwanza nikiri kuwa nimepata taarifa ya changamoto iliyopo baina ya Peter na Erkan na nilichukua hatua ya kuwakutanisha kutafuta muafaka kabla ya kujitokeza mambo ya kuhatarisha amani na kufanyika uhalifu," alisema Ayoub.

Alisema baada ya kuwakutanisha aliwataka kutumia mazungumzo kupitia wanasheria wao kwa sababu serikali haiwezi kuingilia masuala ya biashara na kuwasihi wajiepushe na vitendo vinavyoweza kusababisha uvunjifu wa amani na kuathiri maendeleo ya sekta ya utalii.

Ayoub alisema wakati wakiwa katika mazungumzo kuna kesi imeripotiwa Kituo cha Polisi Kiwengwa kuwa kuna watu zaidi ya 13 (Wamasai) wakiwa na mapanga na marungu kuvamia hoteli hiyo na kupora wageni.

Mkurugenzi wa Kampuni ya Zan Food Trading Limited, Erkan Acikel, alipotakiwa kuzungumzia mgogoro huo na waandishi wa habari hotelini hapo, alikataa kuzungumza chochote kuhusu mgogoro huo.

Hata hivyo, Mkuu wa Wilaya Kaskazini Unguja, Sadifa Juma Khamis, alisema hakuna njia ya kutatua mgogoro wa kibiashara zaidi ya wahusika kutumia vyombo vya sheria kupitia wanasheria wao pamoja na kuheshimu mikataba.

# UTT AMIS ilivyofanya vizuri mwaka 2021

Na Frank Monyo

MKURUGENZI Mtendaji wa Taasisi ya Uwekezaji ya UTT AMIS, Simion Migangala, amesema pamoja na changamoto mbalimbali za kiuchumi kufuatia janga la corona, taasisi hiyo kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, mwaka 2021, imefanya vizuri katika mifuko yake yote.

Amesema Mfuko wa Umoja thamani ya kipande ikiwa imeongezeka kwa shilingi 104.0 na kufikia shilingi 740.0 kwa kila kipande sawa na faida ya asilimia 16.6 kwa mwaka.

Kauli hiyo aliitoa mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam wakati wa mkutano mkuu wa mwaka wa Mifuko ya Uwekezaji ya taasisi hiyo, ambayo ni Mfuko wa Umoja, Mfuko wa Watoto, Hatifungani, Jikimu, Wekeza Maisha na Mfuko wa Jikimu.

Alisema mfuko wa Umoja ni mfuko wa kwanza kuanzishwa na UTT AMIS mwaka 2005 na umeendelea kufanya vizuri kwa muda wa miaka 16 mfululizo kwani mfuko huo ni wa wazi ambao unalenga wawekezaji wenye lengo la muda mrefu na wa kati. Migangala, alisema sera ya uwekezaji katika Mfuko wa Umoja, asilimia mpaka 50 inawekeza kwenye hisa zilizo orodheshwa kwenye soko la hisa la Dar es Salaam na asilimia 50 zilizobaki zinawekezwa katika hati fungani.

"Unaweza kukuta upande wa hisa umefanya vizuri kwa mwaka na upande wa hati fungani nao umefanya vizuri kwa kiwango hiyo kwa mwaka huu wa fedha ulioishia Juni 30, 2021 Mfuko wa Umoja umefanya vizuri sana umekuwa na return sawa na asilimia 16.," alisema Migangala na kuongeza:

"Mwaka ulioishia Juni 30, mwaka 2021, umekuwa ni mwaka mzuri sana kwa taasisi ya UTT AMIS na wawekezaji, mifuko yote imefanya vizuri sana na kupita vigezo ambavyo vimewekwa kupima utendaji wa mifuko."

Alisema kwa upande wa Mfuko wa Ukwasi, ukubwa wa mfuko huo umeongezeka kwa shilingi bilioni 103.1 kutoka shilingi bilioni 112.8 Juni, 2021 hadi shilingi bilioni 215.9 Juni 30, 2021.

Aliongeza kuwa ukubwa wa mfuko uliongezeka kwa shilingi bilioni 103.1 swa na ongezeko la asilimia 91.4, katika kipindi hicho hicho thamani ya kipande iliongezeka kwa shilingi 37.5 sawa na faida ya asilimia 15.3 kwa mwaka.

"Faida ya Mfuko wa Ukwasi kwa kipindi cha mwaka mmoja ni asilimia 15.3 ikilinganishwa na faida ya asilimia 15.1 ulionakiriwa mwaka uliopita 2020. Faida ya asilimia 15.3 ni tafsiri ya ongezeko kwenye mtaji wa mwekezaji aliyewekeza kwa mwaka mmoja," alisema Migangala.

Kwa upande wa Mfuko wa Watoto, Migangala, alisema kuwa hali ya kiutendaji kwa Mfuko wa Watoto ni nzuri na unavutia kwani kwa kipindi cha mwaka mmoja ulioishia Juni 30,2021 faida ni asilimia 19.9.

"UTT AMIS inatambua umuhimu wa mtoto kwa maendeleo ya taifa katika siku zijazo, na kwa sababu hii Mfuko wa Watoto (Watoto Fund) ulizinduliwa kuwa suluhisho la kifedha ambalo linalenga kukuza mtaji wa muda mrefu kwa ajali ya maendeleo ya watoto," alisema.



Mkurugenzi wa Fedha, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), Beatrice Musa-Lupi (kulia), akipokea tuzo ya mshindi wa kwanza ya Umahiri wa Utayarishaji wa Mahesabu kwa mwaka 2020, zilizotolewa na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu Tanzania (NBAA), jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **MPIGAPICHA WETU**

# Wanahisa NICOL wapitisha gawio la bil. 1/-

Na Joseph Mwendapole

WANAHISA wa Kampuni ya NICOL Investment PLC, wameidhinisha gawio la Sh. 1,047, 792, 178 kwa mwaka wa fedha unaoishia 2021 ambapo kwa kila hisa moja itatolewa Sh. 17.

Hayo yalifikiwa mwishoni mwa wiki wakati wa mkutano mkuu wa saba wa mwaka kwa wanahisa wa kampuni hiyo uliofanyika kwenye ukumbi wa Mwalimu Nyerere jijini Dar es Salaam.

Malipo hayo kwa wanahisa kwa mujibu wa mkutano huo yanatarajiwa kulipwa kabla ya tarehe 30 Desemba mwaka huu kwa wanahisa wote walioko kwenye kitabu cha orodha ya wanahisa.

Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu wa Kampuni hiyo, Erasto Ngamilaga, alisema kampuni hiyo ilikuwa katika matatizo siku za nyuma, lakini sasa imeanza kupata mafanikio makubwa na wanahisa wanafurahia manufaa wanayopata.

Alisema kutokana na kazi kubwa iliyofanywa na menejimenti mpya, kampuni hiyo imetangaza kutoa gawio kwa wanahisa wake ambalo litalipwa mwaka huu.

"Tumekuwa na mkutano mzuri ambapo wanahisa wengi wameonyesha kufurahishwa na mwenendo wa kampuni kwa kupata faida kutokana na uwekezaji ilioufanya kwenye maeneo mbalimbali," alisema.

Alisema kampuni inaenda kutekeleza malengo makubwa ya kiuwekezaji kwa kuwekeza kwenye maeneo mengine mengi yenye kuleta faida na kutawanya uwekezaji ili kupata faida.

Alisema kampuni hiyo awali ilikuwa kwenye mlolongo mkubwa wa matatizo ya uongozi wa zamani lakini uongozi mpya umejitahidi kwa kiwango kikubwa kuyatatua na hivi sasa wanahisa wanafurahia matunda.

"Tunaona fahari kwamba wanahisa sasa wanafurahi kwasababu wanapata kile walichokuwa wakistahili na ni matarajio yetu kuwa huko mbele kutakuwa na nuru kubwa sana kwa kampuni kuwa na faida," alisema.

Alisema mwaka 2020 walipendekeza gawio la Sh. 10 kwa kila hisa ambalo kila mwanahisa amelipwa na sasa kutokana na matokeo mazuri ya kifedha kwa kipindi cha nusu mwaka unaoishia tarehe 30 Juni 2021, ambapo faida baada ya kodi iliongezeka hadi Sh. bilioni 3.8 kutoka Sh. bilioni 2.2 mwaka uliopita kipindi kinachofanana.

Alisema faida baada ya kodi kufikia mwisho wa 31 Desemba 2021 inakadiriwa kufikia Sh. bilioni 2.8 na mapato ya msingi kwa kila hisa kuwa karibu ya Sh. 45 kwa kila hisa hivyo kwa kuzingatia mafanikio hayo ndipo waliamua kupendekeza kufanyika malipo ya gawio ya Sh. 17 kwa kila hisa ambayo yataokana na faida ya mwaka wa fedha wa 2021.

Mwenyekiti wa kampuni hiyo, Dk. Gideon Kaunda, aliwaeleza wanahisa wake kuwa kampuni imefanikiwa kukabiliana changamoto mbalimbali na kufanikiwa kushinda kesi zaidi ya 37 ambazo zilifunguliwa dhidi ya kampuni na kuwahakikishia wanahisa kuwa kampuni hivi sasa itaendelea kutoa malipo ya gawio huku thamani ya uwekezaji wetu ikiongezaka.

Wanahisa walipendekeza kuwepo na ongezeko la idadi ya wakurugenzi wa kampuni kutoka idadi iliyopo sasa na kufikia wakurugenzi saba ili kuongeza ufanisi wake wenye kuleta tija.

Katika mkutano huo, wanahisa pia walipendekeza kuanza mchakato wa kujaza nafasi za wakurugenzi hao wapya na wakurugenzi walioomaliza muda wao kufuata taratibu za kuomba kuchaguliwa tena katika mkutano mkuu ujao.

# Ashinda pikipiki kampeni ya Tigo

Mwandishi Wetu

KAMPUNI ya huduma za kidijitali ya Tigo Tanzania, imekabidhi pikipiki moja na simu janja za kisasa kwa washindi wa wiki wa kampeni yake ya mwisho wa mwaka.

Kampeni hiyo inaitwa Wagiftishe - Gift Juu ya Gift, ambapo wateja wanatakiwa kununua ITEL T20 kwa bei ya shilingi 89,000 kutoka duka lolote la Tigo nchini kote ili kupata nafasi ya kujishindia simu janja 504 na pikipiki 1 kila wiki kwa muda wa wiki sita.

Meneja Mawasiliano wa Tigo, Woinde Shisael, jana alitangaza mshindi wa zawadi ya pikipiki wiki hii ambaye ni Noel Kabuje mjasiriamali kutoka Kurasini, Dar es Salaam, na washindi wa simu za kisasa kutoka mikoa mbalimbali nchini.

Akiwapongeza washindi, Shisael alisema: "Kama kinara wa soko katika mabadiliko ya mtindo wa maisha ya kidijitali nchini, Tigo sasa inahakikisha kuwa kila mtu anapata nafasi ya kumiliki simu bora ya kisasa kwa bei nafuu zaidi kwa kila ununuzi wa simu za kisasa za ITEL T20 kutoka kwa maduka ya Tigo nchini kote.

"Wateja waendelee kununua simu za ITEL T20 kutoka maduka ya Tigo nchini kote ili kuingia kwenye droo ya kupata nafasi ya kujishindia moja ya pikipiki 5 na simu janja ambazo bado zinawaniwa katika promosheni hiyo."

Shisael alieleza kuwa mteja anaponunua simu za kisasa aina ya ITEL T20 kutoka duka lolote la Tigo nchini kote, wafanyakazi wa huduma kwa wateja wa Tigo kwenye maduka ya Tigo hurekodi IMEI namba ya simu hiyo, jina la mteja na namba ya simu ya mkononi. Maelezo haya yameingizwa kwenye michoro ya kila wiki. Kila wiki Tigo inatoa zawadi ya pikipiki moja kwa muda wa wiki 6.

Noel Kabuje, aliyejishindia pikipiki alieleza kufurahishwa kwake na zawadi hiyo akisema itamwezesha kuanzisha biashara ya usafiri wa pikipiki (bodaboda).

## DCEA kinara uandaaji taarifa

**Na Gwamaka Alipipi**

MAMLAKA ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA), imeibuka mshindi wa kwanza katika tuzo za umahiri katika uandaaji wa taarifa za fedha, zilizotolewa na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu Tanzania (NBAA).

Utoaji wa tuzo hizo ulifanyika jijini Dar es Salaam na kuhudhuriwa na kampuni, taasisi na mashirika mbalimbali ya serikali na sekta binafsi.

DCEA ilipata tuzo mbili, ya kwanza ni katika kundi la wizara na idara zinazojitegemea ( MDAs) za serikali iliyoandaa vizuri hesabu kwa viwango vya kimataifa kwa sekta za umma (IPSAS) kwa mwaka 2020, ya pili ni mshindi wa jumla kwa MDAs zinazotumia IPSAS kuandaa hesabu zake.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam baada ya kutangazwa kuwa washindi na kupata tuzo hizo, Kamishna Jenerali wa DCEA, Gerald Kusaya, alisema kazi yao siyo tu kudhibiti na kupambana na dawa za kulevya peke yake bali pia inajukumu la kuangalia jinsi ambavyo wanatumia vizuri rasilimali fedha zinatolewa na Rais kuhakikisha zinatumika kama ilivyokusudiwa.

"Haya kwetu ni mafanikio makubwa ambayo yametokana na kuweka vizuri kumbukumbu zetu za mahesabu na ndizo haswa zimetufanya tuwe washindi, DCEA imekuwa ikipata ushindi huo kwa mara nne mfululizo," alisema Kusaya.

Kuhusu ushindi wa tuzo hizo, Kusaya alisema yeye ndiye Mtendaji Mkuu wa Mamlaka hiyo, hivyo anapotoa maelekezo yanasikilizwa na kutekelezwa vizuri zaidi na wale walioko chini yake kwa maana ya wahasibu na watu wote wanaohusika kutunza kumbukumbu ndani ya mamlaka na ndio maana wameendelea kufanya vizuri.

Aidha, alisema jambo la msingi watu lazima wafuate maadili ya watumishi wa umma ikiwa pamoja na taratibu zote za kiofisi.

"Unapokuwa na matumizi mazuri ya kifedha ndio yanayosababisha taasisi kuwa na hesabu nzuri za kifedha, kwa watendaji wakuu tunachotakiwa kufanya kwanza kuifahamu taasisi unayoiongoza na kisha kutoa maelekezo na kuyafauatilia kwa karibu kuona kama yanafanyiwa kazi," alisema na kuongeza:

"Lazima tuzingatie sheria na miongozo ya umma. Malengo ya mamlaka hii ni kuendelea kuibuka na ushindi na kama nilivyotangulia kueleza hii ni mara ya nne mfululizo tunaibuka washindi na kwa jinsi tulivyojipanga na kuweka malengo tutachukua tena mwakani."

# Watafiti wataka sera kulinda sekta isiyo rasmi

**Na Mwandishi Wetu**

UTAFITI wa miaka minne uliofanywa na Chuo Kikuu cha Mzumbe kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Nairobi, Kenya na Roskilde cha nchini Denmark umependekeza kuwapo kwa sera na taratibu madhubuti zitakazosababisha sekta isiyo rasmi kupitia vyama vyao kufaidika na huduma za hifadhi ya jamii.

Malengo makuu ya utafiti yalilenga kufahamu namna wafanyakazi wasio rasmi kwenye sekta za usafiri, ujenzi na wafanya biashara wadogo Kenya na Tanzania wanavyopata huduma rasmi na zisizo rasmi za hifadhi ya jamii, bima za afya, pensheni, fursa za mikopo, mafunzo mbalimbali kama ya afya na usalama na namna vikundi walivyojiundia vinavyosaidia katika juhudi hizo.

Utafiti huo wenye kichwa cha "Sekta Isiyo Rasmi na Hifadhi ya Jamii" ulioanza 2017-2020 ulifadhiliwa na Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Denmark (DANIDA), ulifanywa katika miji na majiji ya Dar es Salaam, Dodoma, Nairobi na Kisumu.

Akizungumza wakati wa warsha ya kuwasilisha matokeo ya utafiti huo kwa wadau mbalimbali jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, Mtafiti na Mratibu Mwandamizi katika Utafiti huo toka Chuo Kikuu Mzumbe, Dk. Godbertha Kinyondo, alisema upo umuhimu kwa taasisi za serikali na wadau kujifunza na kushirikiana na vyama vya wafanyakazi wasio rasmi katika kutunga sera za hifadhi za jamii ili waweze kufaidika na huduma muhimu za kijamii. Alisema ni muhimu sasa kwa serikali kupitia taasisi zake mbalimbali kujenga uwezo na kushirikisha vyama vya wadau hao katika kutunga sera zinazogusa maisha yao na kupitia upya programu za hifadhi za jamii, ili zikidhi mahitaji mapana ya wafanyakazi hao katika sekta isiyo rasmi, hususani ya usafirishaji inayokua kwa kasi Tanzania na Afrika ya Mashariki kwa ujumla.

Mtafiti mwingine wa Chuo Kikuu Mzumbe, Aloyce Gervas, alisema sekta ya ujenzi ni miongoni mwa sekta muhimu katika kuchangia pato la taifa kwa asilimia 13 bado ina watu wasio na ujuzi rasmi na kwamba inaongoza kusababisha ajali za kazini kwa asilimia 23.7 kulinganisha na sekta nyingine.

Alisema upo umuhimu wa kupitia upya sera ya taifa ya sekta ya ujenzi ili kuwatambua vyema mafundi ujenzi wasio na taaluma rasmi na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) kutoa elimu ya kutosha kwa mafundi nchini juu ya faida za mifuko hiyo.

Mtafiti Mwandamizi toka Chuo Kikuu cha Nairobi, Prof. Winnie Mitullah, alisema juhudi za kuboresha sekta isiyo rasmi zinahitaji ushiriki wa wadau mbalimbali na ushirikiano kati ya nchi na nchi ili kufanikiwa.

Naye Mtafiti, Anne Kamau wa Chuo Kikuu Nairobi alisema suala la hifadhi ya jamii kwa sekta isiyo rasmi bado ni changamoto kubwa nchini Kenya na linahitaji mjadala mpana.

Naye Meneja Kitengo kinachoshughulikia sekta isiyo rasmi wa NSSF, Rehema Chuma wa Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) alipongeza juhudi za utafiti huo na kusema tayari shirika hilo linafanya kazi ya kuongeza wigo wa wanachama kupitia sekta isiyo rasmi tangu mwaka 2018.

Naye Mwenyekiti wa Chama Mwamvuli wa Vyama vya Sekta isiyo Rasmi Tanzania (VIBINDO), Gaston Kikuwi, kilichoko na vyama 741 na wanachama zaidi ya 68,000 nchini, alisema mjadala wa huduma za hifadhi ya jamii kwa wafanyakazi sekta isiyo rasmi ni muhimu sana kwa maendeleo ya nchi.

Awali, akifungua warsha hiyo kwa niaba ya Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu Mzumbe, Prof. Lughano Kusiluka; Dk. Mary Rutenge alisema utafiti huo unalenga kuboresha maisha ya wananchi katika nchi hizo mbili ni muhimu na kushauri mamlaka husika kufanyia kazi mapendekezo yake.

Utafiti huo ulihusisha madereva daladala 250, waendesha bodaboda 158 na wajenzi 212 huku upande wa Kenya wafanyakazi 200 wa sekta ya usafirishaji walihusika.



Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni ya Vodacom Tanzania, Sitholizwe Mdlalose (kulia), akionyesha ishara ya upendo, wakati wa uzinduzi wa kampeni mpya msimu huu wa sikukuu ijulikanayo 'Show Love, Tule Shangwe', jijini Dar es Salaam jana, wateja wa Vodacom wataweza kujishindia zawadi mbalimbali wafanyapo miamala ya M-Pesa. Wengine ni Mkurugenzi wa Biashara Vodacom, Linda Riwa (kushoto) na Masta Shangwe. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Asilimia 71 wapata majisafi Songea

**Na Gideon Mwakanosya,**
SONGEA

MENEJA wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Wilaya ya Songea mkoani Ruvuma, Mathias Pangras Charles, amesema asilimia 71 ya wakazi wa wilaya hiyo wanapata huduma ya majisafi.

Pangras amevitaja vijiji ambavyo vinahuduma ya maji, lakini siyo toshelezi ni Mpitimbi 'B', Mbingamharule, Matomondo, Matimira 'A' na 'B', Mpangula, Matomondo, Mhukuru Lilahi na Mhukuru barabarani.

Pangras alielezea mikakati ya kukabiliana na changamoto ya upatikanaji wa huduma ya maji ni uchimbaji wa visima virefu na vifupi na kuendelea na usanifu huduma ya maji ya mtiririko.

Alivitaja vijiji ambavyo vimekosa huduma ya maji ni Makwaya, Mbolongo, Mipeta, Nambendo, Magwamira, Lusonga, Chiulungi, Nakawale, Kituro Lipokera, Maposeni na Morogoro. Vingine ni Mdunduwalo, Kizuka, Magagura, Mpandangindo, Lipaya, Mbilo, Parangu, Lyangwena na Litapwasi.

Pangras aliwataka wananchi kushirikiana na Ruwasa kuibua vyanzo vya maji, badala ya kutegemea wataalam kufika maeneo ya vijijini kutafuta na kubaini vyanzo hivyo jambo ambalo litarahisisha utekelezaji wa miradi.

Halmashauri ya Wilaya ya Songea ina jumla ya vijiji 56 na wakazi wapatao 152,205, kati ya hao wakazi 103,172 wanapata huduma ya majisafi kutoka vyanzo mbalimbali vya maji ambavyo ni visima virefu na vifupi, chemichemi na mito.

Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Brigedia Jenerali Wilbert Ibuge, alikagua vyanzo vya maji kwenye miradi ya maji Ndongosi na Liula wilayani Songea na kuagiza vyanzo hivyo kulindwa ili viwe endelevu.

Brigedia Jenerali Ibuge amesikitishwa na uharibifu wa vyanzo hivyo unaoendelea kufanywa na wananchi kwa kulima mazao na shughuli nyingine za kibinadamu hali inayosababisha vyanzo hivyo kuwa katika hatari ya kutoweka.

Nipashe
Spotika



MAMBO 10 USIYOYAJUA KUHUSU KOCHA RANGNICK UK. 12 - 13



# REKODI 5 ZA MESSI KWA KUTWAA BALLON D'OR

**PARIS,** Ufaransa

LIONEL Messi alishinda tuzo ya Ballon d'Or 2021 baada ya mwaka mwingine wa kuvutia akiwa na klabu na nchi yake.

Messi alitunukiwa tuzo hiyo na mchezaji mwenzake wa zamani wa Barcelona na rafiki yake wa karibu, Luis Suarez baada ya hafla nzuri iliyofanyika kwenye Ukumbi wa Théâtre du Châtelet jijini Paris, Ufaransa.

Messi na Robert Lewandowski walikuwa wanawania tuzo hiyo ya juu zaidi ya mpira wa miguu ya wanaume mwaka huu. Muargentina huyo alishinda Ballon d'Or kwa kura 613 huku Lewandowski akimaliza wa pili kwa kura 580.

Usiku huo pia uliona vipaji vingine kadhaa katika soka vikitambuliwa. Mchezaji nyota wa Barcelona, Pedri alishinda tuzo ya Kopa kwa kuwa mchezaji chipukizi anayekuja kwa kasi zaidi duniani.

Nahodha wa Barcelona wa wanawake, Alexia Putellas alitunukiwa tuzo ya Ballon d'Or kwa wanawake baada ya mwaka mzuri sana ambapo aliisaidia klabu yake kushinda kila taji walilocheza.

Kipa wa Italia na PSG, Gianluigi Donnarumma alitunukiwa tuzo ya Lev Yachine Trophy kwa kuwa mlinda mlango bora.

Tuzo mbili mpya zilianzishwa katika sherehe za Ballon d'Or 2021.

Lewandowski wa Bayern Munich, mfungaji mabao mahiri zaidi duniani katika siku za hivi karibuni, alitunukiwa tuzo ya mshambuliaji Bora wa Mwaka.

Wakati huo huo, Chelsea ilishinda tuzo ya Klabu Bora baada ya mwaka wa kihistoria ambapo timu ya wanaume ilishinda Ligi ya Mabingwa Ulaya, huku timu ya wanawake ikimaliza ya pili.

Mafanikio ya Copa America akiwa na Argentina yalikuwa sababu kuu nyuma ya ushindi wa Messi wa Ballon d'Or.

Licha ya kucheza fainali nne na Argentina hadi 2021, Messi hakuwa na fursa ya kubeba kombe la kimataifa. Hilo lilibadilika mwaka huu, baada ya kuhamasishwa na Nahodha Messi, Argentina iliifunga Brazil katika fainali ya Copa America kule Maracana.

Akiwa na tuzo saba za Ballon d'Or kwa jina lake, Muargentina huyo ndiye anayeshikilia rekodi ya tuzo hiyo kwa kuibeba mara nyingi zaidi.

Makala haya yanaangalia rekodi alizoweka Messi baada ya kushinda tuzo ya saba ya Ballon d'Or, twende sasa...

### #5. WA KWANZA KUSHINDA TUZO SABA

Hadi enzi za Messi na Ronaldo, ni Michel Platini, Johan Cruyff na Marco van Basten pekee ndio waliofanikiwa kushinda tuzo hiyo ya kifahari mara tatu. Messi alikuwa wa kwanza kuvunja rekodi hiyo baada ya ushindi wake wa kihistoria wa mfululizo wa nne kati ya mwaka 2009 na 2012. Messi aliongeza nyingine mwaka wa 2015 baada ya kushinda mataji matatu akiwa na Barcelona.

Ingawa Ronaldo alifikia rekodi ya Messi kwa kushinda Ballon d'Or yake ya tano mwaka 2017, Muargentina huyo aliitwaa tena mwaka 2019. Na sasa amekuwa mchezaji wa kwanza kushinda Ballon d'Or saba.

### #4. WA KWANZA KUSHINDA KUTOKA LIGUE 1

Ingawa mafanikio makubwa ya Messi mwaka huu yalifika akiwa na Barcelona na Argentina, sasa yeye ni mchezaji wa PSG. Sakata kubwa la uhamisho wa majira ya joto, ambapo klabu hiyo ya Catalunya ilishindwa kumbakisha kwa sababu ya matatizo ya kifedha.

Hii ina maana kwamba Messi ni mwanasoka wa pili kutoka Ligue 1 kushinda Ballon d'Or baada ya Jean-Pierre Papin mwaka 1991.

Papin alipata mafanikio hayo ya ajabu kutokana na mwaka wa matokeo makubwa akiwa na Marseille. Mshambuliaji huyo aliisaidia Marseille kufika fainali ya Kombe la Ulaya mwaka huo ingawa walishia kupoteza kwa Red Star Belgrade kwa mikwaju ya penalti.

### #3, MCHEZAJI WA KWANZA WA PSG KUSHINDA

Messi sasa amekuwa mchezaji wa kwanza wa PSG kushinda tuzo ya Ballon d'Or. Kwa PSG, George Weah alikaribia kushinda. Kwa hakika, alishinda Ballon d'Or mwaka 1995, lakini akafanikiwa kuhama kutoka PSG kwenda AC Milan majira ya joto.

Kwa hiyo, alikuwa mchezaji wa AC Milan alipopokea tuzo hiyo. Weah anasalia kuwa mwanasoka pekee wa Afrika kushinda tuzo ya Ballon d'Or.

Katika hotuba yake ya Ballon d'Or, Messi alitaja kwamba analenga zaidi kuendelea kushinda mataji akiwa na PSG na Argentina badala ya kufikiria tuzo ya nane.

### #2. MWENYE UMRI MKUBWA ZAIDI KUSHINDA KARNE YA 21

Akiwa na umri wa miaka 34 na siku 159, Messi pia alikuwa mwanasoka mwenye umri mkubwa zaidi kubeba Ballon d'Or karne hii. Fabio Cannavaro mwaka 2006 na Luka Modric mwaka 2018 walikuwa washindi wa zamani zaidi katika milenia kabla ya Messi. Wote wawili walikuwa na umri wa miaka 33 walipopokea heshima hiyo ya kifahari.

Sir Stanley Matthews pekee ndiye aliye mbele ya mafanikio ya Messi. Matthews, ambaye pia alikuwa mshindi wa kwanza wa Ballon d'Or alishinda akiwa na umri wa miaka 41. Matthews alizingatia sana utimamu wa mwili, na hilo lilimsaidia kuendelea kucheza mchezo huo kwa kiwango cha juu hadi alipokuwa na umri wa miaka 50!

Messi pia ndiye mshindi wa tatu wa tuzo ya Ballon d'Or mwenye umri mdogo zaidi katika historia akiwa na Michael Owen na Mbrazil Ronaldo pekee mbele yake.

### #1. WA KWANZA KUSHINDA BALLON D'OR KATIKA MIONGO MITATU TOFAUTI

Kuwa na uwezo wa kufanya kile anachofanya ni ajabu kutosha na amefanya hivyo kwa kipindi cha miaka 15 mfululizo.

Messi amekuwa mwanasoka bora zaidi duniani tangu mwaka 2007. Alishinda Ballon d'Or yake ya kwanza mwaka 2009.

Messi alitwaa tena Ballon d'Or kutoka kwa Ronaldo mwaka 2015 baada ya kuwa na msimu mgumu akiwa na Barcelona. Kisha akaongeza kombe la sita kwenye mkusanyiko wake na kusonga mbele ya Ronaldo mwaka 2019.

Miaka 12 tangu ushindi wake wa kwanza mwaka 2009, Messi amekuwa mchezaji wa kwanza kubeba Ballon d'Or katika miongo mitatu tofauti. Kimsingi, mabishano yanayohusu mwanasoka bora zaidi katika historia yanaweza kuyumba kati ya Pele, Messi na Maradona. Lakini kwa hakika, Messi amewapita magwiji hao wawili muda mrefu uliopita.

## ISIKUPITE

CRISTIANO Ronaldo ndiye mfungaji wa wakati wote duniani kwa sasa, akiwa amecheka na nyavu mara 801 katika maisha yake soka akifuatiwa na Pele (mabao 765) na Lionel Messi (mabao 756).



# MAMBO 10 USIYOYAJUA KUHUSU KOCHA RANGNICK



**MANCHESTER,** England

RALF Rangnick ameteuliwa kuwa kocha wa muda wa Manchester United. Kocha huyo wa Ujerumani anatarajiwa kuanzisha enzi mpya pale Old Trafford kwa kuendeleza muundo ambao Ole Gunnar Solskjaer ameunda katika klabu hiyo.

**Rangnick amekuwa akifanya kazi kama Mkuu wa Michezo na Maendeleo katika klabu ya Urusi ya Lokomotiv Moscow.**

Baada ya kuhudumu kama kocha wa muda, Rangnick anatazamiwa kufanya kazi kama mshauri katika klabu hiyo kwa kipindi cha miaka miwili. Hii ina maana kwamba, ana uwezekano wa kuwa na uamuzi juu ya nani atakuwa kocha ajaye wa kudumu pale Man United.

Bila shaka, hii ni hatua katika mwelekeo mzuri kwa Man United.

Hapa tunaangalia mambo 10 ambayo huenda huyajui kuhusu Rangnick, haya sasa...

### #10. MVUMBUZI WA 'GEGENPRESSING'

Gegenpressing ni aina ya uchezaji wa timu kwa kusukumiza mashambulizi mbele kwa kasi ambapo timu hujaribu kumiliki tena mpira baada ya kuupoteza. Mfumo huu unahitaji kila mshambuliaji kutafuta mpira wakati timu yao inapoteza umiliki. Huu ndio mfumo ambao Jurgen Klopp ameutumia kwa ufanisi mkubwa pale Liverpool.

Timu zake zinajulikana kwa kucheza soka la kushambulia kwa kiwango cha juu pia na atafaa pale Man United.

### #9. ALIANZA UKOCHA NA MIAKA 25

Rangnick alicheza kwa muda mfupi. Kwa kiasi kikubwa alicheza katika madaraja ya chini nchini Ujerumani na alikuwa na nafasi ndogo katika klabu ya Uingereza ya Southwick alipokuwa akisoma katika Chuo Kikuu cha Sussex.

Akili yake ya busara na kipaji zilibainika mapema na alikuwa kocha wa wachezaji katika klabu ya FC Viktoria Backnang mnamo mwaka 1983.

### #8. ARRIGO SACCHI NDIO MFANO WAKE

Rangnick alikuwa akipokea video za AC Milan ya Arrigo Sacchi iliyotumwa kwake kutoka Italia. Rangnick aliripotiwa kuandika miongozo ya kufundisha wakati huo. Alisoma nafasi ya AC Milan na uchezaji kwa undani sana. Inadaiwa kwamba Rangnick alirudisha nyuma na kutazama mara kwa mara kwa umakini sana video za Milan hadi deki yake ikapasuka.

Sachi aliiongoza AC Milan kwa vipindi viwili kati ya msimu wa 1987-1991 na 1996-1997. Alishinda taji la Serie A msimu wa 1987-88 na pia alishinda mataji ya Ulaya mfululizo. Pia alikuwa kocha wa timu ya Taifa ya Italia iliyomaliza kama washindi wa pili katika Kombe la Dunia la mwaka 1994.

### #7. ALIKATAA KUINOA CHELSEA

Chelsea walikuwa wamemfuata Rangnick walipokuwa wakitafuta kocha wa muda baada ya kutimuliwa kwa Frank Lampard. Hata hivyo, inasemekana Rangnick alikataa nafasi ya kuwa kocha wa muda kwa miezi minne kwa kuwa aliamini angeonekana tu kama 'bata kilema' ambaye huja na kuondoka.

### #6. ALIIPANDISHA TIMU KUTOKA DARAJA LA TATU HADI LIGI KUU (BUNDESLIGA)

Rangnick alikuwa mchezaji wa zamani wa Ulm 1846. Alirejea katika klabu kama kocha mwaka 1997. Rangnick aliipandisha kutoka Daraja la Kwanza hadi Bundesliga 2 kabla ya kuwapeleka kwenye Ligi Kuu ya Ujerumani kwa mara ya kwanza katika historia yao mwaka wa 2000.

### #5. ALIIPANDISHA HANNOVER 96 LIGI KUU (BUNDESLIGA)

Rangnick aliteuliwa kama kocha wa Hannover 96 Mei mwaka 2001. Hannover 96 walikuwa Ligi Daraja la Pili, Bundesliga 2, wakati huo na Rangnick alibadilisha kila kitu. Walishinda taji la Ligi ya Daraja la Pili msimu huo na kupandishwa daraja hadi Bundesliga.

Aliwaongoza kumaliza katika nafasi ya 11 katika msimu wao wa kwanza Bundesliga. Hata hivyo, hawakuweza kuendeleza kiwango chao msimu uliofuata. Hii ilisababisha Rangnick kutimuliwa Machi 2004.

### #4. ALIJIUZULU HOFFENHEIM KWA SABABU YA KUUZWA LUIZ GUSTAVO

Rangnick alipandishwa ngazi baada ya kuchukua mikoba ya Hoffenheim mwaka 2006, na kuwasaidia kufika Bundesliga kwa mara ya kwanza.

Rangnick alichukua nafasi ya ukocha katika klabu ya Hoffenheim msimu wa 2006-07 na kuwatoa kutoka daraja la tatu hadi Bundesliga. Walimaliza katika nafasi ya saba kwenye jedwali la Bundesliga msimu wa 2008-09.

Hata hivyo, Rangnick alijiuzulu baada ya klabu hiyo kumuuza kiungo Luiz Gustavo kwa Bayern Munich bila yeye kujulishwa. Hoffenheim walikuwa wa nane kwenye Bundesliga, Rangnick aliposajiliwa kama kocha baada ya ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Borussia Monchengladbach msimu wa 2010-11.

### #3. ALIIPANDISHA RB LEIPZIG LIGI KUU (BUNDESLIGA)

Rangnick alitengeneza kupanda kwa RB Leipzig hadi kileleni mwa Bundesliga. Baada ya Alexander Zorniger kujiuzulu kama kocha mkuu, alitangaza kuchukua nafasi hiyo msimu wa 2015-16. Aliipandisha hadi Bundesliga kabla ya kumruhusu Ralph Hassenhuttl kuchukua mikoba mwaka 2016.

Rangnick alikuwa kocha wa RB Leipzig kwa mara nyingine tena Julai 2018. Aliiongoza timu hiyo kumaliza katika nafasi ya tatu kwenye Bundesliga na pia kuwapeleka hadi fainali ya DFB Pokal ambayo walipoteza kwa Bayern Munich.

### #2. AMEMFUNDISHA THOMAS TUCHEL

Rangnick alimfundisha Thomas Tuchel kama mchezaji wa Ulm. Mnamo Februari, Rangnick alisema hivi kuhusu Tuchel:

"Thomas (Tuchel) alikuwa kocha kupitia kwangu. Alikuwa mchezaji wangu kule Ulm na ilimbidi asitishe kuendelea kucheza kwa sababu ya matatizo ya goti. Nilimpa kazi kama kocha wetu wa vijana chini ya umri wa miaka 15. Hakuwa na nia ya kuwa kocha, alikuwa akifanya kazi katika baa moja huko Stuttgart."

### #1. MSHAURI WA TUCHEL NA KLOPP

Rangick alikuwa kocha wa FC Schalke wakati kocha wa sasa wa Liverpool, Jurgen Klopp aliposhinda taji lake la kwanza la Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, akiwa na Borussia Dortmund. Klopp amemzungumzia sana Rangnick siku za nyuma na hata kusema anaweza kuwa kocha bora wa Ujerumani.

Tuchel, Klopp, Ralph Hassenhuttl na Julian Nagelsmann wote ni makocha wanaomchukulia Rangnick kama mmoja wa washauri wao.

## Nukuu


"Sina uhakika kwa asilimia 100 kuhusu tuzo ya Ballon d'Or, mara zote anapewa Messi [Lionel] na sina tatizo na hilo, lakini kama huwezi kumpa Robert Lewandowski wakati huu baada ya kuwa na mwaka bora, kwa haika kabisa inashangaza. Na Mo [Salah] alitakiwa kuwa kwenye nafasi ya juu zaidi. Ilinishangaza na nafasi aliyokuwapo," **Kocha wa Liverpool, Jurgen Klopp.**



"Thierry Henry na mimi [Alan Shearer], tunaweza kufikia idadi ya mabao [801] ya Ronaldo [Cristiano] ikiwa tu tutachanganya mabao yetu yote na yele tuliyofunga kwenye mazoezi," **nguli wa soka wa zamani wa England, Alan Shearer.**



"Mimi hushinda tuzo ya Ballon d'Or kwanza kibinafsi na pili kwa klabu ninayoichezea. Napigania kushinda taji hilo kwangu mimi binafsi na kwa wale wanaonipenda, sipiganii kushinda dhidi ya mtu mwingine," **mshambuliaji wa Manchester United, Cristiano Ronaldo akipinga kauli kuwa lengo lake ni kushindana na Messi katika kutwaa tuzo hiyo.**



Nipashe
Spotika





Frank Ngailo akimtoka beki wa Cameroon kwenye mechi ya CANAF iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa wiki iliyopita. **NA MPIGAPICHA WETU**

# FRANK NGAILO: NYOTA TEMBO WARRIORS NA NDOTO KOMBE LA DUNIA

**Na Saada Akida**

KWA miaka kadha iliyopita hadi sasa kuna baadhi ya familia huwaficha ndani watoto wenye ulemavu kwa kuona aibu, hivyo kushindwa kuwapa elimu na kuendeleza vipaji walivyonavyo.

Kila mwenye ulemavu awe amezaliwa nao au amekutana ameupata ukubwani, hakosi kuwa na kipaji ama uwezo wa kufanya kazi fulani kuonyesha kitu kwa maslahi yake hata ya kitaifa.

Hili linadhihirika kupitia timu ya Taifa ya Tanzania ya Soka kwa watu wenye ulemavu, 'Tembo Warriors', baada ya kulishangaza taifa kwa kuliwakilisha vema kwenye michuano ya Mataifa Afrika kwa wenye ulemavu wa viungo (CANAF), kwa kufuzu kwenda kucheza Kombe la Dunia mwakani nchini Uturuki.

Tembo Warriors ni miongoni mwa timu nne za Afrika zilizokata tiketi hiyo pamoja na Angola, Ghana, Liberia, huku straika Mtanzania Frank Cassian Ngailo akiibuka mchezaji bora wa michuano hiyo iliyomalizika nchini mwishoni mwa wiki kwa Waghana kutwaa ubingwa baada ya kuwachapa Waangola 3-2.

Tanzania imeshika nafasi ya nne baada ya kukubali kichapo cha mabao 4-0 kutoka kwa Liberia kwenye mechi ya kusaka mshindi wa tatu huku mwanafainali mwingine, Ghana ikishika nafasi ya pili.

Hata hivyo, Ngailo ameacha alama katika mashindano hayo kwani mbali na kuwa mchezaji bora, lakini ndiye aliyeibeba Tanzania kufuzu Kombe la Dunia baada ya kuifunga Sierra Leon katika mechi ya mwisho ya hatua ya makundi na kisha robo fainali kufunga tena dhidi ya Cameroon na kutinga nusu fainali.

Ngailo ambaye alizaliwa Septemba 6, mwaka 2000, akiwa na ulemavu wa mguu ni mtoto wa kwanza katika familia ya mzee Cassian Ngailo na mkewe Yusta, wakiwa watoto watano katika familia yao, wanaume watatu na wanawake wawili, kati ya hao yeye pekee ndiye mwenye ulemavu.

Hata hivyo, pamoja na kuzaliwa na ulemavu huo, Ngailo anasema baba na mama yake hawakujisikia unyonge, kwani walishikana bega kwa bega kuhakikisha anapata elimu na kufikia malengo yake ikiwamo kukuza kipaji chake cha kucheza soka.

## ELIMU

Ngailo anasema elimu yake ni kidato cha nne aliyopata katika Shule ya Sekondari Pugu, wakati shule ya awali alisoma Kimbili wilayani Ludewe hadi darasa la pili baada ya hapo akapata udhamini kupitia Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), ambapo lilimleta Dar es Salaam na kupelekwa shule ya Ukovu kuanza tena upya darasa la kwanza hadi la saba.

"Nilifanikiwa kumaliza darasa la saba katika shule ya Ukovu nikapata bahati ya kuchaguliwa Sekondari ya Pungu na kusoma hapo hadi kidato cha nne, baada ya hapo sikutaka kuendelea kwa sababu ya soka," anasema Ngailo.

## MAISHA YA SOKA

Anasema anacheza katika klabu ya L.S.Llester Senior inayocheza Ligi ya Tanzania kwa watu wenye Ulemavu, na kwamba kipaji chake cha soka alianza kukionyesha tangu akiwa darasa la nne.

Anasema soka la ushindani alianzia tangu mwaka 2015 baada ya kwenda sekondari na kukutana na wenzake wenye ulemavu, wakawa wanacheza dhidi ya wanafunzi wenzao ambao hawakuwa na ulemavu.

## NAFASI ANAZOCHEZA

Ngailo anasema ana uwezo wa kucheza kama mshambuliaji, kiungo na beki wa pembeni hiyo ikitokana na mchezo huo kutumia wachezaji sita ndani.

"Awali nilikuwa nacheza kama kipa muda wote nikiwa katika mashindano ya UMITASHUMTA, niliamua kuachana na nafasi hiyo kwa sababu nilikuwa natumia mguu wa bandia, lakini nilipofika sekondari nilihamia nafasi ya ndani," anasema.

Anasema mwaka 2014 baada ya kuacha kutumia mguu wa bandia alipewa magongo na kuanza kujifunza kucheza nafasi za ndani lakini hadi mwaka 2015 anamaliza darasa la saba bado alikuwa anacheza kama kipa.

## CHANGAMOTO

Anasema kwa upande wa familia yake hakuweza kupata changamoto yoyote kwa sababu baba, mama pamoja na ndugu zake walimpa hamasa kubwa kwa kumtia moyo anaweza kufikia malengo yake.

"Upande wa familia yangu sikuwahi kupata shida ikiwamo kutengwa kutokana na hali yangu, kazi kubwa nilikuwa nikipata nje ya familia yangu kwa vijana ambao nilikuwa nafanya nao mazoezi.

"Kuna siku niliumia sana wakati niko kwenye mazoezi na vijana wenzangu ambao si walemavu, ilitokea bahati mbaya nilimgonga mwenzangu na hizi fimbo (Gongo) tunazotumia kwa msaada wa kutembea, alichukia na kutoa maneno si ya kiungwana na kunipokonya gongo na kulitupa nje, niliumia sana na sikwenda kufanya nao mazoezi tena," anasema.

## SIRI YA KIPAJI

"Nilikuwa napenda sana kucheza soka, nikiwa nasoma sekondari niliomba Mungu ashushe miujiza yake kuwapo na mchezo wa mpira wa miguu kwa ajili ya watu wenye ulemavu.

"Nashukuru Mungu akaitika kilio changu na mwaka 2018 walikuja watu kutoka nchi ya Uholanzi, wakiwa na lengo la kuutangaza na kusambaza mchezo wa soka la walemavu ili kujulikana.

"Walitoa mafuzo kwa walimu na kuleta vifaa vya kucheza mchezo huo, kwa kipindi kifupi walichokuja wageni hao kuliandaliwa ligi, nilifanya vizuri na kupata nafasi ya kwenda mazoezi na kisha kwenda Uturuki, lakini walimu wangu walinizuia kwa sababu kipindi hicho walipenda nisome kwanza. Nilikubaliana nafasi hiyo nikaitoa kwa mtu mwingine," anasema.

## TUZO YA MCHEZAJI BORA CANAF, CECAFA

Anasema mbali na kutwaa tuzo msimu huu katika michuano ya CANAF yaliyomalizika wiki iliyopita, alishafanikiwa pia kupata tuzo katika michuano ya CECAFA na mara tatu akichukuwa mchezaji bora wa ligi ya Tanzania akiwa katika klabu yake ya L.S.L lester Senior huku wakiwa mabingwa mara tatu mfululizo.

## KOMBE LA DUNIA

"Serikali iendelee kutusapoti kwa kila hali, kazi kubwa itakuwa kwetu wachezaji kwenda kupambana kuipeperusha vema bendera ya nchi na kuifanya Tanzania kuwa miongoni mwa mataifa ambayo yanatajwa katika michezo ikiwamo soka la walemavu," anasema.

## USHAURI

Anasema michuano ya CANAF imeonyesha jinsi gani watu wenye ulemavu wanaweza kufanya kitu na kuisaidia jamii au kuleta mafanikio katika nchini, hivyo wazazi na walezi waachane na mila potofu kuhusu kuwazuia ama kuwaficha watoto wao wenye ulemavu kuonyesha vipaji vyao.

## JE, WAJUA?



USHINDI wa mabao 3-2 iliyoupata West Ham dhidi ya Chelsea mwishoni mwa wiki, unaifanya klabu hiyo kuibakiza Arsenal tu kabla ya kukamilisha kuvinyuka vigogo vyote vya sita bora Ligi Kuu England msimu huu; Liverpool ilipigwa 3-2, Man City ikapigwa 2-1, Tottenham ikalambwa 1-0 huku Man United nayo ikinyukwa 1-0.







Mkuu wa Wilaya ya Chemba, Saimon Chacha, akimsaidia mmoja wa watu wenye ulemavu, Abenel Festo (13), mkazi wa kijiji cha Chambalo wilayani Chemba baada ya kumkabidhi baiskeli zilizotolewa kwa msaada na Bodi ya Nafaka na Mazao Mchangayiko Tanzania kwenye maadhimisho ya Siku Kimataifa ya Watu wenye Ulemavu, iliyofanyika kimkoa viwanja vya Shule ya Msingi Chemba juzi. Watatu kulia ni Meneja wa Utawala wa bodi hiyo, mkoani Dodoma, Amisa Shabani. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Mradi wajenga shule 225 za sekondari

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

JUMLA ya Sh. bilioni 130.5 zimetolewa kwa ajili ya ujenzi wa shule za sekondari 225 kupitia mradi wa kuboresha elimu ya sekondari nchini (SEQUIP).

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Nteghenjwa Hosseah, alibainisha hayo juzi kwenye taarifa yake iliyotolewa kwa vyombo vya habari jijini hapa.

Alisema, Ofisi ya Rais imepeleka kiasi cha Sh. bilioni 100.58 kwa ajili ya ujenzi wa shule za sekondari mpya 214 ambazo zitajengwa kwenye kata za majimbo yote nchini.

Pia alisema kiasi cha Sh. bilioni 30, zimepelekwa kwa ajili ya ujenzi wa shule za sekondari mpya za wasichana kwenye mikoa 10 Tanzania Bara.

"Mradi huu wa SEQUIP unatekelezwa kwenye eneo la Elimu ya Sekondari kuanzia kidato cha kwanza hadi ya sita kwa muda wa miaka mitano kuanzia mwaka wa fedha 2020/21 - 2024/25 na utekelezaji wake umeelekezwa kwenye maeneo ya vipaumbele vya serikali.

Alisema maeneo hayo ni yale yanayogusa moja kwa moja elimu ya sekondari ambayo ni pamoja na ujenzi wa shule mpya za sekondari zipatazo 1,000 zitakazojengwa katika kata ambazo hazina shule za sekondari.

"Pamoja na maeneo ambayo yana wanafunzi wengi ukilinganisha na miundombinu iliyopo na ujenzi wa shule mpya za sekondari za wasichana za mikoa 26 ambapo katika kila mkoa itajengewa shule moja," alisema.

Alisema ujenzi wa shule hizo utakua unafanyika kadri fedha zitakavyokuwa zinapatikana na kwa sasa wanaendelea na uchambuzi ili kujenga shule za nyongeza 20 kwenye kata zenye msongamano wa wanafunzi.

"Gharama ya ujenzi wa shule za sekondari za kata ni Sh. milioni 600 kwa kila shule na kiasi kilichopelekwa katika awamu hii ya kwanza ni Sh. milioni 470," alisema.

Vilevile, alisema gharama ya ujenzi wa shule za sekondari za wasichana za mikoa ni Sh. bilioni nne ambapo kiasi cha Sh. bilioni tatu kimetolewa ikiwa ni malipo ya awamu ya kwanza ya ujenzi kwa kila shule.

Alisema, shule za sekondari za kata zitakuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi wasiopungua 400 kuanzia kidato cha kwanza hadi cha nne na shule za wasichana za mikoa zitachukua wanafunzi wasiopungua 1,000 kwa kila shule.

"Mradi huu wa SEQUIP umelenga kuongeza fursa ya upatikanaji wa elimu ya sekondari, kuweka mazingira salama ya elimu kwa wasichana na kuhakikisha wanafunzi wote wanapata elimu bora ya sekondari," alisisitiza.

Alisema, kutokana na upelekaji wa fedha hizo Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Ummy Mwalimu, alitoa maelekezo kwa wakuu wa mikoa na wakurugenzi wote wa halmashauri.

Alisema, maelekezo hayo ni pamoja na halmashauri zote zihakikishe kuwa maeneo yaliyoteuliwa kwa ajili ya ujenzi wa shule hizo hayana migogoro ya umiliki wa ardhi.

Pia halmashauri za majiji na manispaa ambazo zina ufinyu wa maeneo ya ujenzi wanaruhusiwa kutumia ramani za ujenzi wa ghorofa ambapo halmashauri husika zinatakiwa kuomba kibali cha kutumia kiasi kilichotengwa na mapato ya ndani kuweza kukamilisha ujenzi wa shule husika.

"Maelekezo mengine ni halmashauri zilizopatiwa fedha za ujenzi zinatakiwa kuanza ndani ya wiki mbili baada ya kupokea fedha na mwongozo wa ujenzi na kukamilika katika kipindi cha miezi sita," alisema.

# Viongozi ushirika wapewa jukumu kusaka masoko ya mazao

**Na Paul Mabeja, DODOMA**

VIONGOZI wa vyama vya ushirika nchini wametakiwa kutafuta masoko ya mazao mbalimbali yanayozalishwa kwenye maeneo yao ili kuwawezesha wakulima kupata uhakika wa masoko yenye tija kwao na taifa kwa ujumla.

Mrajis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika, Dk. Benson Ndiege, alibainisha hayo wakati akizungumza kwenye mafunzo ya Masoko na Biashara kwa viongozi na watendaji wa vyama vya ushirika.

Dk. Ndiege alisema viongozi wa ushirika wana wajibu wa kuwasaidia wakulima kutafuta fursa za masoko ya mazao yao hali itakayo wasaidia kuendelea kupata bei zenye ushindani.

Aliongeza kuwa hivi sasa ni wakati wa viongozi kushirikiana na wadau kuongeza thamani ya mazao kupitia uchakataji na uwekezaji wa viwanda ili kupanua wigo wa masoko.

"Ni wakati sasa kwa viongozi kuhakikisha mnatumia fursa mbalimbali za kujitangaza, kushirikiana na wadau wengine wa ndani na nje ya nchi ili wakulima wetu wapate masoko ya bidhaa zao na tusiishie kuuza bidhaa ghafi bali tujielekeze kwenye bidhaa zilizoongezwa thamani," alisema.

Pia alisema mafunzo hayo ya biashara na masoko yanalenga kuwaongezea uwezo viongozi na maofisa masoko wa vyama vya ushirika kupanua wigo wa utafutaji wa masoko ili wakulima waendelee kunufaika.

Aidha, alisema Tume itaendelea kuhakikisha mafunzo hayo yanakuwa endelevu.

Akichangia mada katika mafunzo hayo mwakilishi wa Taasisi ya Sekta Binafsi (TPSF), Victoria Michael, alisema vyama vya ushirika vina fursa kubwa ya kuongeza pato la kwa kufufua viwanda vingi zaidi vitakavyosaidia kuongeza mnyororo wa thamani ya mazao kama vile korosho na kahawa yanayosafirishwa ng'ambo.

Vilevile, alisema uongezaji wa thamani pamoja na ufungashaji mzuri wa bidhaa za mazao unaongeza na kuitangaza nchi kimataifa.

Kaimu Meneja Mkuu wa Mradi wa Pamoja wa Vyama vya Vikuu vya Tumbaku (T.C.J.E), Bakari Kassia, kwa niaba ya washiriki alisema mafunzo hayo yatawawezesha kupanua fursa za masoko kupitia mada zilizoangazia mifumo ya masoko ya ushirika, masoko ya kimkakati, kilimo cha mkataba.

Kadhalika, aina ya minada ya uuzaji wa mazao, namna bora ya kufikia masoko ya nje ya nchi kwa kushirikisha serikali na balozi zilizopo katika mataifa mbalimbali.

Mafunzo hayo yalihudhuriwa na wenyeviti, mameneja na maofisa masoko 145 kutoka mikoa mbalimbali, ambao ni watendaji muhimu katika uuzaji wa mazao ya wakulima katika vyama vya ushirika.

# Bosi TBA aridhishwa ujenzi nyumba za serikali

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KAIMU Mkurugenzi wa Idara ya Miliki Wakala wa Majengo Tanzania (TBA), Said Mndeme, ameeleza kuridhishwa na kasi ya ujenzi wa mradi wa nyumba 3,500 na nyumba 20 za viongozi zinazojengwa jijini Dodoma na Wakala huo.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi jijini Dodoma baada ya kukagua ujenzi wa nyumba hizo, alisema ameridhishwa na namna wakala huo ulivyojipanga kutekeleza miradi hiyo kwa kuwa na vifaa vya kutosha na vya uhakika.

"Tumeridhika kwa jinsi ambavyo wamejipanga tuna saruji ya kutosha na nondo za haya ni maono ya wakala, hatuna sababu ya kuwa na vikwazo vyovyote binafsi... nimeridhika na nimefurahi katika kuhakikisha tunapunguza gharama na ubora unakuwa mzuri mashine ya kisasa ya kuchakata zege.

"Tumeona kiwanda kingine cha uzalishaji wa tofali hii itatusaidia tofali zenye ubora tumeambiwa kiwanda kinauwezo wa kuzalisha tofali 6,000 kwa siku."

Alisema mradi wa Nzuguni unaenda kwa kasi ambapo amedai awamu ya kwanza zinajengwa nyumba 150 na hadi sasa nyumba takribani 86, zimeanza kujengwa.

"Nyumba hizi 3,500 zitakuwa ni za kisasa kutakuwa na ujenzi maghorofa 100 na nyumba kubwa 200 na nyumba za saizi ya kati 1400, maghorofa yatakuwa nyumba tofauti tofauti 800 na za size za chini nyumba 1,000,"alisema.

Aidha, alisema katika eneo hilo kutakuwa na huduma za kijamii ambapo kutajengwa shule za awali tano, nyumba za ibada misikiti na makanisa, soko na kituo cha biashara.

Kuhusu nyumba 20 za viongozi katika eneo la Kisasa jijini Dodoma, Mndeme alisema zimeboreshwa na kuongezewa ubunifu ikiwa ni pamoja na vyumba vyote vitakuwa na vyoo vya ndani.

"Lakini tumeona jitihada kubwa ambazo zimefanyika nyumba hizi zinajengwa katika nyumba 300 katika eneo la Kisasa, lakini nyumba hizi sasa hivi zimeboreshwa kwa kiasi kikubwa kwanza nyumba hizi muonekano ni tofauti na zile nyumba 300 ambazo zilijengwa za sasa hivi kila chumba kina choo,"alisema.

Kaimu Meneja Maendeleo ya Miliki TBA, Suzan Ulula, alisema wanaamini watafikia malengo ambayo wamejiwekea ikiwa ni pamoja na kukamilisha kwa wakati ujenzi wa nyumba hizo.

"Baada ya kutembelea Nzuguni na Kisasa tunaamini tutafikia malengo wakala ambayo imeyaweka kwa watumishi wa serikali kwa mkoa wa Dodoma tuna maeneo mengine Iyumbu na katika mikoa mbalimbali Arusha na Dar tunategemea tutaendelea na sehemu zingine," alisema.





## Katibu mkuu aagiza vituo bunifu vyuoni

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

KATIBU Mkuu, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto (Idara ya kuu ya Maendeleo ya Jamii), Dk. John Jingu, ameagiza kuanzishwa kwa vituo bunifu kwa kushirikisha jamii katika vyuo vyote vya maendeleo ya jamii nchini.

Dk. Jingu amesema lengo ni kuwandaa vijana kujiajiri wanapohitimu na si kupoteza elimu wanayoipata.

Dk. Jingu alitoa kauli hiyo juzi mkoani Mbeya wakati wa kongamano la wanafunzi lililoandaliwa na Chuo cha Maendeleo ya Jamii kilichoko Uyole jijini Mbeya.

Alisema umefika wakati kwa vyuo vyote kuwa na mifumo ya ubunifu ili kuondokana na tatizo la ajira nchini kupitia programu mbalimbali zitakazojikita kutoa mafunzo ya namna ya kujikwamua na umaskini.

Alisema kuwa mafanikio makubwa yanatokana na ushirikishwaji wa jamii katika kubuni miradi shirikisha ambayo italeta tija kubwa na kuwezesha serikali kutambua changamoto na kuzitatua katika nyanja mbalimbali kikiwepo kilimo na ufugaji.

Dk. Jingu alisema serikali kwa kutambua mchango mkubwa wa vyuo hivyo na jamii kwa ujumla imeweka mipango mikakati ya kuhamasisha vikundi vitakavyoanzishwa vinapatiwa mikopo kupitia katika halmashauri asilimia 10 ili viweze kujiendesha na kujiinua kiuchumi.

"Kwenye vyuo vyote vya Maendeleo ya Jamii katika baadhi ya mikoa kumeanzishwa vituo ubunifu ambavyo vitakusanya mawazo ya wanafunzi na Jamii na kuchakata ili kuibua fursa ambazo zinakuwa chachu na kuleta mafanikio, " alisema.

Akizungumza kwa niaba ya Katibu Tawala Mkoa wa Mbeya, Stella Kategile, alisema kuwa wamepokea maelekezo ya wizara na kwamba jamii imekuwa ikishirikishwa hususan katika kampeni za lishe, ulinzi wa mama na mtoto, ukatili wa kijinsia, na kuhamasisha katika shughuli za maendeleo ya kiuchumi.

Mwanafunzi wa Chuo cha Maendeleo ya Jamii jijini humo, Meshack Japheth, alisema kuna kila sababu ya kuishukuru serikali ilipolifikisha taifa kwa kuwekeza katika nyanja mbalimbali katika sekta ya elimu, jambo ambalo lilikuwa ni ndoto kwa kipindi cha miaka 60 ya uhuru wa Tanzania Bara.

# Watatu mbaroni tuhuma utapeli mitandaoni kujiita Freemason

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya limewakamata watuhumiwa watatu wanaojihusisha na utapeli kwa njia ya mitandao ya kijamii wakijifanya wanatoa utajiri kupitia Jumuiya ya Freemason.

Kwa mujibu wa Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoani Mbeya, Ulrich Matei, watuhumiwa hao walikamatwa Desemba mosi 2021 majira ya mchana katika eneo la Kiwira, wilayani ya Rungwe baada ya kufanya msako unaoendelea dhidi ya wahalifu kwa njia ya mitandao ya kijamii.

Alisema watuhumiwa hao katika nyakati tofauti walitumia mitandao ya kijamii ya Facebook na Instragram kufanya utapeli wakijifanya kuwa wanatoa utajiri kupitia jumuiya ya Freemason.

Aliwataja watuhumiwa hao ni Elia Ngulwa (24), mfanyabiashara, mkazi wa Uyole, Innocent Kyando (21) mjasiriamali na mkazi wa Kiwira na Shaban Ibrahim (20), mkazi wa Itezi Mashariki - Uyole.

Kamanda Matei alifafanua kuwa watuhumiwa hao walitekeleza uhalifu huo kati ya Agosti 23 2021 na Novemba 29, mwaka huu na kufanikiwa kumtapeli Mariam Josephat (25), mfanyabiashara wa eneo la Kitangiri jijini Mwanza kiasi cha shilingi milioni 106 na fedha hizo zilitumwa kwa nyakati tofauti kwenye simu za watuhumiwa wakidai wanataka kufanya matambiko mbalimbali kama Mtandao wa Freemason unavyotaka.

Aidha, katika tukio hilo, watuhumiwa walikutwa wakiwa na simu tano za mkononi za aina mbalimbali ambazo zilizitumika kutapeli watu kupitia mitandao ya kijamii ya Facebook na Instagram.

Alisema upelelezi washauri hilo unaendelea na baada ya kukamilika, watuhumiwa watafikishwa mahakamani.

Katika hatua nyingine, mtuhumiwa wa dawa za kulevya, Simeon Faducuane (44), raia kutoka Msumbiji, amehukumiwa kwenda jela miaka 20 au kulipa faini ya shilingi bilioni moja baada ya kukutwa na hatia ya kusafirisha dawa za kulevya aina ya Heroine Hydrocloride gramu 812 zikiwa na thamani ya Sh. milioni 365.

Kamanda Matei alisema Novemba, 30 mwaka huu, katika Mahakama Kuu ya Kanda ya Mbeya, mtuhumiwa alipatikana na hatia baada ya kukiri kosa la kusafirisha dawa hizo.

Matei alisema Mahakama iliamuru mshtakiwa huyo kutumikia kifungo cha miaka 20 jela au kulipa faini ya shilingi bilioni moja sambamba na gari alilotumia kusafirishia dawa za kulevya kutaifishwa na serikali.

"Wakati wa kutekeleza majukumu yetu Jeshi la Polisi kupitia misako na doria mbalimbali tulifanikiwa kumkamata Faducuane eneo la mpaka wa Kasumulu wilayani Kyela akiwa na gari aina ya Mitsubishi Pajero namba MLK 5535 ikiwa na dawa za kulevya aina ya Heroine Hydrochloride zenye uzito wa gramu 8120.69," alisema Kamanda Matei.




Katibu Mkuu, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Idara ya Kuu ya Maendeleo ya Jamii, Dk. John Jingu, akizungumza na watumishi pamoja na wanafunzi wa Chuo cha Maendeleo ya Jamii kilichoko Uyole jijini Mbeya mwishoni mwa wiki. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Vyuo vya elimu vyatakiwa kutoa mafunzo kwa wenye mahitaji

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

SHIRIKA la Child Support Tanzania (CST), linajihusisha na kuhamasisha utoaji wa Elimu Jumuishi kwa Shule mbalimbali za Msingi jijini Mbeya, limeomba serikali kuhakikisha vyuo vyote vya ualimu vinatoa mafunzo maalum ya namna ya kufundisha watoto wenye mahitaji maalumu.

Lengo ni wanapohitimu wawe na ujuzi pamoja na utayari wa kufundisha kundi hilo kuliko ilivyo sasa ambapo hulazimika kupata mafunzo upya.

Ombi hilo lilitolewa mwishoni mwa wiki na Mkurugenzi wa CST, Noela Msuya, wakati wa maadhimisho ya Siku ya Watu wenye Ulemavu Duniani ambayo yalienda sambamba na mahafali ya watoto wenye mahitaji maalum waliohitimu mafunzo ya awali kuingia darasa la kwanza.

Msuya alisema licha baadhi ya vyuo vya walimu kutoa mafunzo kwa ajili ya kuwafundisha watoto wenye mahitaji maalum lakini uhitaji ni mkubwa sana hivyo serikali haina budi kutoa mafunzo hayo kwa vyuo vyote vya walimu nchini ili kuwasaidia watoto wenye ulemavu kusoma kwenye mazingira mazuri kupitia programu ya elimu jumuishi.

Alisema kutokana na uhaba wa walimu wa kufundisha watoto wenye mahitaji maalum kupitia mpango wa elimu jumuishi CST imekuwa ikitoa mafunzo maalum kwa walimu namna ya kuwafundisha watoto hao.

"CST tumejikita kuwahudumia watoto wenye ulemavu nchini ni baada ya kuona wanapata vikwazo mbalimbali ikiwamo kufungiwa ndani na kukosa haki ya kupata elimu, matibabu na huduma nyingine kupitia programu yetu ya peleka marafiki zangu wote shule tumeweza kuwafikia watoto wengi," alisema Msuya.

Aliongeza kuwa hadi sasa jumla ya watoto 600 wamefikiwa na programu hiyo kupitia shule 30 za msingi mkoani Mbeya, na kwamba lengo lao ni kuzifikia shule zote nchini.

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, Kaimu Tawala, Vincent Mbua aliwataka wananchi kutoa taarifa kwa serikali dhidi ya wale wote wanaowaficha watoto wenye ulemavu ndani.

Alisema yeyote atakayebainika hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yake na kwamba lengo la msisitizo huo ni kuwahakikisha watoto wenye ulemavu wanapata haki ya elimu kama walivyo wengine.

Aidha, alilishukuru CST kwa kujikita kuwasaidia watoto wenye ulemavu kwa kuanzisha shule yao yenye mahitaji maalum pamoja na kuendesha programu mbalimbali zinazohamasisha kuwapeleka watoto wenye ulemavu shuleni.

Alisema serikali inaendelea kuboresha miundombinu ya elimu kwa kuhakikisha inakuwa rafiki kwa watoto wenye ulemavu na





# Othman: Serikali inasimamia maslahi ya wenye ulemavu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, amesema serikali inasimamia maslahi ya watu wenye ulemavu katika nyanja tofauti kwa nia ya kutoa fursa zaidi za maendeleo.

Othman ameyataja baadhi ya mambo ambayo kuwa ni suala la elimu ya kuwajengea uwezo mkubwa zaidi.

Othman aliyasema hayo juzi huko Nungwi Wilaya ya Kaskazini 'A' Unguja katika maadhimisho ya kilele cha Siku ya Watu Wenye Ulemavu Duniani.

Alisema kupitia Wizara ya Elimu ya Zanzibar, serikali imeanzisha mfumo wa shirikishi na mjumuisho wa elimu ili kuwapatia fursa kubwa za stadi za maisha sambamba na kutoa nafasi za uongozi kwa watu wenye ulemavu Zanzibar.

Alifahamisha kwamba katika jitihada za kuendelea kutoa fursa kwa watu wenye ulemavu hivi karibuni, serikali itaanzisha ujenzi wa shule maalum, jambo ambalo linaongeza juhudi katika kuongeza mslahi ya watu wenye ulemavu Zanzibar.

Aidha, alisema kwamba serikali imeimarisha mazingira bora ya kusaidia na kushajiisha washirika wa maendeleo ili kuwasaidia zaidi watu wenye ulemavu jambo ambalo linakwenda sambamba na juhudi za dunia za kuwatetea watu wenye ulemavu kupitia maazimio mbalimbali ambayo yanaongeza nguvu katika kuingiza masuala ya watu wenye ulemavu katika masuala tofauti ya nchi.

Alisema Serikali ya Zanzibar kwa kushirikiana na jumuiya ya kimataifa inaendelea na michakato mbalimbali ya kuimarisha sera na sheria zinazosimamia maslahi ya watu wenye ulemavu, jambo ambalo limesaidia kuanzishwa kwa Baraza la Watu wenye Ulemavu Zanzibar chombo ambacho ni muhimu katika kusimamia na kutetea haki zao.

Alisema kwamba serikali inajitihadi kuwa na sheria bora za kulinda maslahi ya watu wenye ulemafu pamoja na kuweka mkazo mkubwa wa usimamizi wake ikiwamo kushuriki katika masuala ya siasa katika kuweka ushirikishwaji sawa na kujengwa miundombinu rafiki kwa jamiii hiyo ili Zanzibar kuwa nchi ya mfano katika kulinda maslahi ya watu wenye ulemavu.

Aliwakumbusha viongozi na Jumuiya ya Watu wenye Ulemavu Zanzibar kujiandaa kuhesabiwa katika sensa ya mwaka 2022, ambayo itasaidia kupaanga masuala mbalimbali ikiwamo maslahi ya watu wenye ulermavu.

Aidha, aliwakumbusha kinamama kwenda hospitali mapema kuchunguzwa afya za watoto na wale ambao watakuwa wamepata watoto wenye ulemavu athari za ulemavu zitaweza kupunguzwa iwapo wamewahishwa hospitali.

Pia Othman aliwataka wanajamii kuacha tabia iliyojengeka ya kusababisha ongezeko la ajali kwa ajali za barabarani zinazotokana na uzembe kwa kutozingatiwa ipasavyo kanuni na sheria za usalama barabarani.

Naye Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Dk. Saada Salum Mkuya, alisema kwamba takwimu zinaonyesha kuwa Zanzibar ina asilimia 5.8 ya watu wenye ulemavu wa aina mbalimbali na takwimu hizo zinaweza kuongezeka kwa kuwa watu wengi hawajajitokeza na taarifa zao kufahamika.

Mwenyekiti wa Baraza la Taifa la Watu Wenye Ulemavu Zanzibar, Salma Saadat, alipongeza juhudi za serikali katika kuhakikisha maslahi ya watu wenye ulemavu yanazingatiwa na kulindwa na kuwataka wanajumuiya hizo kuhakikisha wanaongeza ushirikiano katika kudai haki zao.



Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, akimkabidhi baiskeli ya magurudumu matatu Miza Wanje Khamis, Uwanja wa Hamboru Nungwi Kaskazini A Unguja katika kilele cha maadhimisho ya Siku ya Watu wenye Ulemavu Duniani, yaliyofanyika kitaifa Zanzibar juzi. Kulia ni Mkurugenzi wa Baraza la Watu wenye Ulemavu, Ussi Khamis. **PICHA: RAHMA SULEIMAN, ZANZIBAR**

## Krismasi kuleta neema ya watalii

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MENEJA wa Hoteli ya Marumaruko iliyopo Mji Mkongwe Zanzibar, amesema Sikukuu ya Krismasi ya mwaka huu wanatarajia kupokea wageni wengi kutokana na mikakati mbalimbali inayofanywa na serikali katika kukabiliana na janga la ugonjwa wa covid-19.

Alisema miongoni mwa mikakati hiyo ni uhamasishaji wa chanjo ya corona ili kudhibiti maambukizi ya ugonjwa huo, hali ambayo imepelekea uingiaji watalii kutoka mataifa mbalimbali duniani baada ya nchi zao kuondoa vikwazo vya safari kutoka taifa moja kwenda lingine.

Meneja huyo aliyasema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari Mjini Zanzibar ambapo alisema Sikukuu ya Krismasi ya mwaka jana hawakupata watalii kutokana na vizuwizi vilivyotokana na ugonjwa wa corona.

"Tunashukuru mwaka huu hali ni shwari, watalii wanaingia kwa wingi Zanzibar ambapo sekta ya utalii imeanza kuimarika baada ya kutetereka kutokana na corona," alisema.

Alisema zaidi ya wageni 150 wanatarajiwa kufika katika hoteli hiyo kwa ajili ya msimu wa sikukuu kwa kula na kunywa pamoja na kufanya ibada ya Krismasi.

Meneja huyo aliwataka wananchi kuendelea kuchanja chanjo ya corona ili kudhibiti maambukizi, ili Zanzibar ipate watalii wengi, na kwamba wafanyakazi wa hoteli hiyo wameshachanja.

Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Jinsia,Wazee na Watoto, Nassor Ahmed Mazrui, alisema wananchi watakapojikinga na corona, uchumi unaimarika kwa sababu watalii na wawekezaji wataingia nchini baada ya kuona nchi ipo salama.

"Wimbi la nne la corona tusiliogope, tulikabili kwa kujikinga na Ishallah tutavuka salama kama tulivyovuka katika wimbi la kwanza, la pili na la tatu," alisema Mazrui.

# Jamii yaombwa ushirikiano kuukomesha udhalilishaji

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Uchumi wa Bluu na Uvuvi, Abdalla Hussein Kombo, ameitaka jamii kushirikiana katika kuondoa vitendo vya udhalilishaji nchini, kwa sababu vimekuwa vikiongezeka siku hadi siku.

Alieleza hayo Kikwajuni Zanzibar wakati akifungua kongamano la vijana la kuadhimisha Siku 16 za harakati za Kupinga vitendo vya Ukatili na Udhalilishaji.

Alisema wazazi, walezi pamoja na walimu wa shule na madrasa wana jukumu la kusimamia vyema malezi ya watoto kwa kuwalea katika malezi yenye maadili mema ili kuepukana na vitendo viovu vya udhalilishaji.

Aidha, aliwataka vijana kuachana na tabia ya kukaa vijiweni, jambo linapelekea ushawishi wa kufanya vitendo visivyofaa kwa jamii, badala yake wajiunge na vikundi vya ujasiriamali ili kujipatia mahitaji yao ya lazima. Pia alieleza kuwa vijana wengi wamekuwa wakijishughulisha sana na mitandao kwa kuperuzi na kuangalia picha za ngono sambamba na mambo ya wasanii ambayo yanapotosha utamaduni wetu yakiwamo mavazi.

Naye Mkurugenzi wa Elimu Mbadala na Watu Wazima, Mashavu Ahmada Fakih, alisema wazazi hawapaswi kuwafungisha ndoa watoto wakiwa katika masomo, jambo ambalo hupelekea kupoteza malengo yao ya baadae. Alieleza kuwa hivi karibuni wamesitisha ndoa za wanafunzi watano, ambao bado wanaendelea na masomo yao.

Vilevile, aliwataka wanafunzi kujitambua wanapokuwa shuleni na kuwa makini na masomo ili kufikia malengo waliyojiwekea hapo baadaye.

Aliwashauri wanafunzi kujishughulisha na shughuli mbalimbali ikiwamo ufundi na biashara mara tu wamalizapo masomo ili wajipatie kipato halali na kuepukana na suala zima la udhalilishaji.

Akitoa takwimu ya vitendo vya udhalilishaji kutoka Januari hadi Novemba mwaka huu, aliesema Wilaya ya Magharibi "A" inaongoza kuliko wilaya zote kwa kuwa na kesi 260 ikifuatiwa na Wilaya ya Magharibi "B" ambayo ina jumla ya kesi 243.

Kongamano hilo lilojumuisha vijana na wadau mbalimbali wa kupinga vitendo katili na udhalilshaji liliandaliwa na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa- Kitengo cha Wanawake (UN WOMEN).

# Serikali yaipongeza sekta binafsi kukuza uchumi, ajira

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa ameipongeza sekta binafsi inavyoshiriki kukuza uchumi wa nchi ikiwamo kutoa fursa za ajira kwa Watanzania kupitia kampuni na mashirika.

Alitoa pongezi hizo juzi katika hafla ya chakula cha jioni iliyoandaliwa na Jumuiya ya Watendaji Wakuu wa Kampuni na Mashirika (CEO Roundtable of Tanzania), jijini Dar es Salaam.

Waziri Mkuu ambaye alimwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan, alisema kuwa moja ya mafanikio makubwa ni kuongezeka kwa ajira kutoka milioni 20.5 mwaka 2014 hadi milioni 24.1 mwaka 2020/2021 na kuongezeka kwa kwenye sekta isiyo rasmi kutoka asilimia 22.0 mwaka 2014 hadi asilimia 29.4 mwaka 2020/2021.

Alisema licha ya changamoto ya UVIKO-19, Tanzania imeendelea kufanya vizuri kwenye sekta nyingine za kiuchumi na kutoa ajira katika sekta ya kilimo, hali ambayo inaashiria mwelekeo mzuri katika utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano unaolenga kuwa na asilimia 60 ya ajira kwenye kilimo ifikapo mwaka 2025/2026.

"Serikali itaendelea kuchukua hatua madhubuti za kuimarisha uwekezaji, biashara na kuongeza wigo wa vyanzo vya mapato kwa kushirikiana na sekta binafsi. Hatua hizo zimechangia kwa kiasi kikubwa kuongezeka kwa uwekezaji nchini hususan kutoka nje ambao kati ya Machi na Agosti, 2021 ulifikia takribani Dola za Marekani bilioni tatu."

Waziri Mkuu alisema Rais Samia ameendelea kuimarisha mazingira bora ya uwekezaji na ufanyaji wa biashara na anaamini kupitia mkutano huo watatoa ushauri na mapendekezo ya namna bora ya kuimarisha shughuli za biashara na uwekezaji.

Kadhalika, alisema serikali ina matarajio na sekta binafsi kuwa itaendelea kuunga mkono jitihada zake katika kupambana na kupunguza hewa ya ukaa na matumizi ya plastiki.

"Ongezeni uwekezaji kwenye miradi ya matumizi ya nishati mbadala, ustawishaji wa misitu na utunzaji wa mazingira na usafirishaji kwa kutumia teknolojia za kisasa zisizozalisha hewa ya ukaa," alisema na kuongeza:

"Nitoe wito kwenu mwendelee kuwaita wawekezaji waje hapa nchini na kuwekeza katika sekta mbalimbali za kilimo, utalii na nishati."

Katika hatua nyingine, Waziri Mkuu ameitaka sekta binafsi iweke kipaumbele na kuzingatia usawa wa kijinsia katika utoaji wa ajira hasa wanawake ili kuunga mkono jitihada za serikali.

Alisema katika mwaka 2020/2021, ukosefu wa ajira kwa wanawake upo juu zaidi ikilinganishwa na wanaume, wanawake wasiokuwa na ajira wanafikia asilimia 12.7 na wanaume ni asilimia 5.8.

Naye Mwenyekiti wa CEO Roundtable of Tanzania, Sanjay Rughani, aliipongeza Serikali ya Awamu ya Sita kwa namna inavyoshirikiana na sekta binafsi katika kuweka mazingira mazuri ya ufanyaji biashara na kuahidi kuwa watahakikisha kupitia shughuli zao, wanaifanya Tanzania ikue kiuchumi si tu Afrika bali duniani kwa ujumla.



Waziri wa Nishati, January Makamba (wapili kushoto), jana aliongoza matembezi ya hisani yaliyoandaliwa na Taasisi isiyo ya Kiserikali ya Volunteers In Development (VID) kwa lengo la kuwasaidia watoto yatima yenye kauli mbiu ya 'Tutembee, Tuwasaidie Yatima ni Jukumu Letu'. **NA MPIGAPICHA WETU**

## NIT, SSCS kuboresha sekta usafiri, usafirishaji

**Na Prosper Makene**

CHUO cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) kimeingia katika makubaliano na Kampuni ya Simba Supply Chain Solutions (SSCS) ili kuongeza idadi ya wataalamu wabobezi katika sekta ya usafiri na usafirishaji.

Wakizungumza baada ya kusaini makubaliano hayo mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam, Mkuu wa Chuo cha NIT, Prof. Zacharia Mganilwa na Mkurugenzi Mkuu wa kampuni ya SSCS, Hussein Dewji walisema makubaliano hayo yatasaidia kwa kiasi kikubwa kuboresha taaluma katika sekta ya usafiri na usafirishaji.

Prof. Mganilwa alisema kuwa kupitia makubaliano hayo, Kampuni ya SSCA itatoa mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi wa Chuo cha NIT, hivyo kuhitimu kama wataalamu wabobezi kwenye sekta nyeti ya usafiri na usafirishaji.

"Madhumuni makuu ya makubaliano haya ni kuimarisha uhusiano kati ya NIT na Simba Supply Chain Solution katika kuboresha ujuzi wa wanafunzi na wafanyakazi katika maeneo ya usafirishaji," Prof. Mganilwa alisema.

"Tumeingia makubaliano katika maeneo 11 ambayo ni mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi, mafunzo kwa wafanyakazi, kubadilishana utaalamu, ziara za mafunzo ama masomo na vile vile kukuza uhusiano wa wafanyakazi," alisema.

Aliyataja maeneo mengine ya ushirikiano ni utafiti na ushauri, utoaji wa mafunzo ya udereva kwa kampuni ya SSCS pamoja na kuwajengea uwezo madereva wa kampuni hiyo.

Meneja Mkuu wa SSCS, Ajuaye Msese, alisema kampuni yake imekubali kutoa nafasi za mafunzo kwa vitendo ikiwa ni pamoja na kutoa fursa ya ziara za masomo na uhusiano kwa wafanyakazi na wanafunzi.

# Tiketi za mtandao usafiri mabasi zapigiwa chapuo

**Na Beatrice Shayo**

WATANZANIA wanaotumia usafiri wa mabasi ya abiria wametakiwa kununua tiketi za mabasi hayo kwa njia ya mtandao, kupitia mfumo wa tiketi rafiki uliyozinduliwa mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam.

Akizungumza wakati wa uzinduzi huo, Mkurugenzi wa Kampuni ya Global Light, Raymond Magambo, alisema mfumo huo umekuwa ukipigwa vita na mawakala wanaodhani wanakwenda kuchukuliwa kazi zao lakini jambo hilo si kweli kwani watakwenda kufanya kazi pamoja.

Alisema mfumo huo utaenda kuboresha kiwango cha utoaji huduma katika sekta ya usafirishaji wa abiria kwa njia ya mabasi kwa kuwezesha kuwa na njia rahisi, salama na yenye uhakika kwa watoa huduma kufanya shughuli zao kirahisi.

Hata hivyo alisema mchakato wa kuja na maombi hayo uliwachukua miaka sita kutokana na baadhi ya mambo ya kiufundi kutokamilika kwa wakati.

"Dunia sasa inafanya kazi kwa kutumia teknolojia ya kidijitali, halikadhalika, mabasi ya abiria yaendane na mabadiliko ya teknolojia kwa kufanya kazi kidijitali," alisema.

Alisema mchakato huo ulianza mwaka 2015, walilazimika kukamilisha baadhi ya mambo ya kiufundi ya serikali kwa kuhakikisha wanazingatia sheria na taratibu zitakazohakikisha mfumo utakapoanza na serikali itaweza kupata mapato yake.

"Tatizo jingine ni changamoto za mfumo wa kuhakikisha wamiliki wa mabasi yaendayo mikoani wanapata fedha zao kupitia teknolojia hiyo bila matatizo yoyote," alisema.

Alisema abiria wataweza kununua tiketi zao kupitia tovuti (online), simu na sehemu ya mauzo kwa wateja wanaonunua tiketi kupitia mawakala.

Wakati huo huo, Ndamba Trans, Mkurugenzi wa mabasi ya Ndamba Trans inayofanya safari zake kutoka Dar es Salaam hadi Lindi, Musa Ngambo, alisema wamiliki wa mabasi wapo tayari kuunganishwa na mfumo huo.

Alisema wana amini mfumo huo utafanya miamala yote kwa uwazi na kuwawezesha wamiliki wa mabasi kupata malipo yao halisi.

## Mjumbe NEC CCM amwaga kadi 10,000

**Mwandishi Wetu,** SIMIYU

MJUMBE wa Halmashauri Kuu Taifa (NEC) wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Mkoa wa Simiyu, Emmanuel Gungu, ametoa kadi 10,000 kwa ajili ya wanachama, zitakazotolewa kwa wilaya tano za mkoa huo.

Gungu alitoa kadi hizo, mbele ya maofisa wa Idara ya Oganization ya chama hicho kutoka Makao Makuu ya Chama Dodoma ambao walifanya ziara mkoani Simiyu, kwa lengo la kutoa elimu mbalimbali kwa wanachama ikiwamo namna ya kusajili kwa kutumia mfumo wa kidigitali.

Akizungumza katika kikao cha Halmashauri Kuu ya Chama hicho, Wilaya ya Bariadi, Gungu alisema lengo la kutoa kadi hizo ni kuhakikisha CCM Mkoa wa Simiyu inaongeza idadi ya wanachama na kukiimarisha vema chama ndani ya mkoa huo.

Akizungumza na mwaandishi wa habari hizi jana, Gungu alisema ma yeye kama mwanachama na kiongozi ana jukumu la kuhakikisha kwa kushirikina na viongozi wengine wanakiimarisha chama hicho, ikiwamo kuhakikisha kila mwanaCCM anakuwa na kadi ya chama.

"Ni jukumu, letu wanaCCM kuhakikisha kila mwanachama anakuwa na kadi ya chama, hivyo nimeamua kutoa kadi 10,000. Hii inamaana kwamba kila wilaya ndani ya Mkoa wa Simiyu itapata kadi 2,000," alisema Gungu.

## SBL: Tutaunga mkono ajenda wenye ulemavu

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Bia ya Serengeti (SBL) imeungana na mataifa mengine duniani kuadhimisha Siku ya Kimataifa ya Watu Wenye Ulemavu Duniani (IDPD) 2021, huku ikiahidi kuunga mkono mapambano ya haki za watu wenye ulemavu.

Akizungumza jijini Dar es Salaam wakati wa kuwasha taa za dhambarau katika jengo la makao makuu ya kampuni hiyo ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya IDPD, Mkurugenzi Mtendaji wa SBL, Mark Ocitti, alisema ajenda ya ujumuishi na watu wenye ulemavu inapewa kipaumbele kikubwa katika SBL.

Mark alisema SBL ni muumuni mkubwa wa fursa na haki sawa kwa wote na kuongeza kuwa katika kuhakikisha inaishi kwa vitendo kwenye hilo, imejiwekea nguzo tatu zinazowawezesha kutekeleza ajenda ya watu wenye ulemavu.

# Ashauri mitaala ilenge kutengeneza ajira

**Na Julieth Mkireri,** BAGAMOYO

KATIBU Mtendaji wa Baraza la Mitihani Tanzania, Dk. Charles Msonde, ameelekeza uongozi wa Chuo cha Ukutubi na Uhifadhi Nyaraka (SLADS), kuhakikisha mitaala inayotumika kutolea mafunzo inalenga kuwatengeneza watendaji kazi za ufundi mgumu na laini wanaoweza kujiajiri na kuajiriwa.

Dk. Msonde alitoa maelekezo hayo mwishoni mwa wiki alipokuwa katika mahafali ya 27 ya chuo hicho, Bagamoyo na kusema mafunzo hayo yatasaidia kupunguza tatizo la ajira nchini.

Alisema ni muhimu mitaala ya mafunzo iendane na mahitaji ya soko la ajira, lakini pia mabadiliko ya kijamii kiuchumi na kiteknolojia.

"Ifahamike kwamba jukumu la vyuo vya kati ni kutoa taaluma inayolenga kutengeneza watendaji wa kazi za ufundi mgumu na laini katika sekta mbalimbali wanaoweza kuajiriwa na kujiajiri, napenda kuuhimiza uongozi wa chuo kuhakikisha mitaala ya kutolea mafunzo inaweza kufikia malengo," alisema.


Dk. Msonde aliwasisitiza wahitimu kuondokana na utegemezi wa wazazi na badala yake kutumia fursa zilizopo kwa kufanya shughuli halali na kuondokana na dhana kwamba lazima ajira zitoke serikalini.

Mwenyekiti wa Baraza la chuo hicho, Dk. Mboni Ruzegea, alisema lengo la chuo hicho ni kutoa mafunzo bora kwa wanachuo ili kuwezesha kupata wataalamu wabobezi katika fani ya ukutubi watakaoleta tija kwa kutoa huduma bora.

Dk. Mboni alisema Bodi ya Huduma za Maktaba kupitia Wizara ya Elimu imejipamga kuendelea kuboresha miundombinu na rasilimali watu katika chuo hicho ili kuendana na kasi ya ukuaji wa sayansi na teknolojia na mahitaji ya soko la ajira nchini.

Kaimu Mkuu wa Chuo, Victoria Kessy, alisema wanakabiliwa na vikwazo mbalimbali ikiwamo kukosekana kwa maktaba ya kisasa kutokana na iliyopo kutotosheleza idadi halisi ya wanachuo waliopo na utoaji wa mafunzo ya kisasa ya ukutubi.

Alitaja vikwazo vingine kuwa ni ukosefu wa vyombo vya usafiri, miundombinu dhaifu ya TEHAMA, kukosekana kwa ukuta wa kuzunguka eneo la chuo kwa kampasi ya Bagamoyo na upungufu wa kambi za mihadhara na vyumba vya madarasa.




Jengo la Makao Makuu ya Kampuni ya Bia ya Serengeti (SLB) lililoko jijini Dar es Salaam, liliwashwa taa za zambarau ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Watu Wenye Ulemavu Duniani. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Jafo aridhishwa utekelezaji miradi

**Na Mwandishi Wetu,** SIMANJIRO

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Selemani Jafo, amesema ameridhishwa na utekelezaji wa miradi ya kuhimili mabadiliko ya tabianchi wilayani Simanjiro mkoani Manyara.

Jafo alitoa kauli hiyo jana alipozuru kikazi wilayani humo kukagua miradi hiyo inayotekelezwa na Ofisi ya Makamu wa Rais kupitia fedha za Mfuko wa Mazingira Duniani (Global Environmental Facility) chini ya Mradi wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi kwa kutumia Mifumo Ikolojia (EBARR).

Katika ziara hiyo ndani ya Wilaya ya Simanjiro, Jafo alitembelea mradi wa ufugaji wa mbuzi, mradi wa birika la kunyweshea ng'ombe, mradi wa josho la kuogeshea ng'ombe, mradi wa kuku chotara pamoja na mradi wa kiwanda cha ngozi.

Waziri huyo alieleza kufurahishwa na utekelezaji wa miradi hiyo iliyozingatia mahitaji halisi ya jamii sambamba na thamani ya fedha, huku akiagiza miradi hiyo yote iwe imekamilika na kuzinduliwa ndani ya mwezi ujao.

Alisema miradi ya kuhimili mabadiliko ya tabia nchi imekuwa ikitekelezwa na Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kuibuliwa na wananchi katika maeneo husika na imekuwa ni msaada mkubwa katika jamii.

Miradi hiyo inatekelezwa katika halmashauri za wilaya tano za Simanjiro, Kishapu, Mpwapwa, Mvomero na Wilaya ya Kaskazini A Unguja. Miradi hiyo ya kuhimili mabadiliko ya tabianchi inagharimu dola za Marekani milioni 7.5, sawa na wastani wa Sh. bilioni 17.4 kwa wilaya zote tano.

Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro, Dk. Suleiman Serera, alishukuru Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kuja na mradi huo wilayani humo na kusema imekuwa ni msaada mkubwa kwa wananchi. Alisema kuwa siri ya mafanikio katika kutekeleza miradi hiyo ni uwapo wa watumishi wanaojitambua katika kuisimamia, hali inayosaidia uongozi kuwasimamia vizuri.

# TANZANITE NA MATUMAINI KUITOA BURUNDI KUFUZU KOMBE LA DUNIA

**Na Saada Akida**

BAADA ya kukiongoza kikosi chake kuibuka na ushindi wa mabao 3-2 dhidi ya Burundi, Kocha Mkuu wa Timu ya Taifa ya Tanzania chini miaka 20 'Tanzanite', Bakari Shime, amesema kazi iliyopo mbele yake sasa ni kujipanga kwenda kutafuta matokeo mazuri kwenye mechi ya marudiano ugenini dhidi ya Warundi hao kuwania kufuzu Kombe la Dunia mwakani nchini Costa Rica, America Kusini.

Wakati Shime akiyasema hayo, Kocha Mkuu wa Burundi, Danielle Niyibimenya, alisema katika mechi hiyo iliyopigwa Uwanja wa Azam Complex, Chamazi nje kidogo ya Jiji la Dar es Salaam, ilikuwa ngumu kipindi cha kwanza na ana matumaini mchezo ujao kwenye ardhi ya nyumbani kwao, watakuwa imara zaidi na kupata matokeo.

Makocha hao wakizungumza baada ya dakika 90 za mchezo huo kukamilika, Shime alisema mchezo haukuwa kama walivyotarajia baada ya kukwama kwa mpango wao wa pili kuzuia wapinzani wasipate nafasi ya kufunga na mabeki kuruhusu mabao mawili.

**Alisema mbali na kushindwa kuwazuia lakini wamefanikiwa kwenye mpango wao wa kwanza kwa kupata ushindi wa mabao mengi na kukamilika kwa mchezo wakiwa wanaongoza 3-2.**

"Mipango yetu ni kufunga mabao mengi, tulishindwa kuzuia hasa kipindi cha pili tulikata moto na wachezaji wangu kuingiwa na uoga na kuwapa nafasi wapinzani wetu kutushambulia, wamezitumia vizuri nafasi walizotengeneza na kupata mabao mawili.

"Kitu ninachokiamini, tunaweza kufunga kokote, kikubwa ni kuhakikisha naifanyia kazi safu yangu ya ulinzi ili tunapokwenda katika mchezo wa marudiano tukatafute ushindi na kuweza kulinda kwa kutoruhusu kufungwa jambo linalowezekana," alisema Shime.

Lakini Kocha wa Burundi, Danielle alisema mchezo ulikuwa mzuri katika vipindi vyote viwili, Tanzania wakinufaika kipindi cha kwanza pia wao walicheza vizuri kipindi cha pili na kuweza kupata mabao mawili.

"Wachezaji wangu walikuwa na uoga, hivyo kupoteza kipindi cha kwanza baada ya hapo niliwapa maelekezo na kufanyia kazi kasoro nilizozibaini, hivyo tukapata mabao mawili. Tunarudi nyumbani kufanyia kazi mapungufu yetu kuhakikisha tunaenda kupata ushindi katika uwanja wa nyumbani," alisema Daniella wakati huu timu hizo zikitarajiwa kurudiana baada ya wiki mbili.



Rais Mstaafu wa Awamu ya Nne, Dk. Jakaya Kikwete (katikati), Mkuu wa Idara ya Taasisi za Serikali na Taasisi Binafsi wa Benki ya NMB, William Makoresho (wapili kushoto mbele) na Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Prof. William Anangisye (kulia), wakiwaongoza wanamichezo kufanya mazoezi ya viungo kabla ya kuanza rasmi kutimua mbio za kilometa tano katika Mbio za Hisani za UDSM zilizofanyika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Benki ya NMB ilishiriki kama mdhamini mkuu katika mbio hizo. **NA MPIGAPICHA WETU**

## Nyota wa Simba Queen aenda kukipiga Uturuki

**Na Adam Fungamwango**

MCHEZAJI wa timu ya soka la wanawake ya klabu ya Simba, Simba Queens, Mawete Musolo, amejiunga na klabu ya Bitexen Adana Idman Yurdu ya nchini Uturuki, baada ya kuitumikia timu hiyo kwa msimu mmoja.

Mtandao wa Instagram wa klabu hiyo ya Simba, umeonyesha picha za mchezaji huyo na kumtakia kila la kheri kwenye klabu yake mpya na maisha mapya.

"Kwa niaba ya uongozi wa Simba, pamoja na wachezaji, benchi la ufundi, mashabiki, tunakutakiwa kila la kheri katika maisha yako mapya ndani ya klabu ya Bitexen Adana Idman Yurdu ya Uturuki.

"Simba tunaendelee kukushukuru kwa mchango wako ndani ya timu yetu kwa kipindi cha mwaka mmoja tulichokuwa pamoja, hatuna cha zaidi. Simba ni nyumbani kwako, muda na siku yoyote unakaribishwa," uliandika mtandao huyo wa Klabu ya Simba Qeens.

Mawete anayecheza nafasi ya kiungo mshambuliaji, raia wa Kidemokrasia ya Congo, alijiunga na timu hiyo baada ya viongozi wa Simba kumwona kwenye mechi ya kusaka tiketi ya kufuzu michuano ya Olimpiki iliyofanyika Tokyo nchini Japan mwaka jana, timu ya Taifa ya Wanawake ya Congo ilipocheza dhidi ya Twiga Stars 2019 Uwanja wa Benjamin Mkapa na kutoka sare ya mabao 2-2.

Kwa muda mfupi tu alitokea kuwa kipenzi cha mashabiki wa timu hiyo kutokana na kipaji na uwezo wake mkubwa wa kupiga chenga, nguvu na kufunga mabao, akiisaidia Simba Queens kutwaa ubingwa wa Tanzania Bara msimu uliomalizika.

# Mdundo yazindua Shindano la ma-DJ 2021

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI inayoongoza kwa huduma mtandaoni barani Afrika ya Mdundo, imezindua shindano la Ma-DJ, lenye lengo la kutoa fursa kwa Ma-DJ nchini kuonyesha umahiri na vipaji vyao.

Shindano hilo, mbali na kutoa mwanya kwa Ma-DJ kuonyesha umahiri wao, pia litakuwa ni fursa kwa wananchi mbalimbali kupata uelewa kuhusiana na Kampuni ya Mdundo ambayo inafanya kazi na wasanii wenye vipaji wakiwamo wanamuziki zaidi ya 100,000 barani Afrika.

Meneja Masoko wa Kampuni ya Mdundo, William Abagi, alisema kampeni hiyo ya mwezi mmoja, itawahusisha ma-DJ wa aina zote ambao alisema watatakiwa kuwasilisha na kuweka kazi zao (mixtapes) kwenye mtandao wa Mdundo kabla ya Desemba 10, mwaka huu.

Alisema Tanzania iliongoza kwa idadi ya watumiaji wa muziki ya Mdundo huku ikiwa na watumiaji zaidi ya milioni 4.1 katika robo ya mwaka hadi kufikia Septemba mwaka huu huku akibainisha kuwa hii ni fursa nzuri kwa ma-DJ kutumia nafasi hii kujisajili ili watangaze kazi zao na kuongeza idadi ya mashabiki.

Kwa mujibu wa Abagi, DJ atakayeshinda atapata udhamini wenye thamani ya shilingi milioni saba, nusu saa ya kuonyesha umahiri wake kwenye tukio mojawapo kubwa katika moja ya hafla kubwa mwakani, pamoja na muda kwenye redio, huku mshindi wa kampeni hiyo akitarajiwa kutangazwa Desemba 22, mwaka huu.

"Tumeshirikiana na kampuni ya Vodacom Tanzania kuwapa wapenzi wa muziki fursa ya kupata maudhui ya muziki wa hali ya juu kutoka kwa ma-DJ mahiri kwa bei ya chini ya hadi Sh. 100," alisema.

Abagi alisisitiza kuwa washiriki walio na nia wanapaswa kufuata maelekezo kupitia mitandao ya kijamii ya Mdundo kwa maelezo zaidi, ambayo alisema ni pamoja na; Instagram: @mdundomusicTz, facebook: @mdundomusic, Twitter: @Mdundotanzania.

Kampuni ya Mdundo inajivunia watumiaji zaidi ya milioni 10.5 kwa mwezi, walioko katika Mataifa ya Tanzania, Kenya, Nigeria, Ghana na mengine yaliyoko barani Afrika, ambapo inafanya kazi na zaidi ya wanamuziki 100,000 wenye asili ya Afrika.

## ZISIKUPITE

### LINGARD ATAKIWA

KLABU ya Newcastle United imeanza kuonyesha nia ya kumtaka kiungo wa England, Jesse Lingard, katika dirisha dogo la Januari, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, mkataba wake unatarajiwa kuisha katika kipindi cha majira ya joto. ***(Times)***

### ARTETA AMTAKA TOURE

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta amesema kuwa yupo tayari kusaidiana na nyota wa zamani wa Manchester City, Yaya Toure ili wainoe pamoja timu hiyo. Toure mwenye umri wa miaka 38, kwa sasa yupo kwenye klabu ya Tottenham. ***(Sunday Mirror)***

### EMENALO AIKATAA NEWCASTLE

MKURUGENZI wa michezo wa zamani wa Chelsea, Michael Emenalo, ameitupilia mbali ofa ya kuwa mkurugenzi ndani ya Newcastle. ***(Sunday Telegraph)***

### MOURINHO ATAJWA EVERTON

HUENDA Everton ikamchukua kocha wa zamani wa Chelsea na Manchester United, Jose Mourinho, ambaye kwa sasa anainoa Roma, maamuzi hayo yatafanyika mpaka waanze mchakato wa kumwondoa kocha wa sasa, Rafael Benitez. ***(Daily Star on Sunday)***

### HAALAND KUONDOKA

KIONGOZI Mkuu wa Borussia Dortmund, Michael Zorc, amemruhusu nyota wa Norway, Erling Braut Haaland mwenye umri wa miaka 21, kuondoka. ***(Sunday Mirror)***

### DEMBELE MAMBO SAFI

BARCELONA imeonyesha nia ya kumpa ofa nono winga wao, Ousmane Dembele mwenye umri wa miaka 24. ***(Marca)***

### JUVE, PSG NAZO ZAJITOSA

KLABU ya Juventus nayo imeanza mchakato wa kumtaka nyota wa Barcelona, Ousmane Dembele, lakini Paris St-Germain imeonyesha utayari wa kumtaka mchezaji huyo. ***(Sport)***

### KULUSEVSKI AGOMBEWA

KLABU za Arsenal na Totttenham zimeonyesha utayari wao wa kutaka kumsajili kiungo wa kati wa Juventus, Dejan Kulusevski mwenye umri wa miaka 21, huku wakimtaka kwa mkopo raia huyo wa Sweden ***(Calciomercato, via Football Italia)***

### SPURS YABISHA HODI BARCA

KLABU ya Tottenham imeungana na Manchester United pamoja na Newcastle United katika kuitaka saini ya Ousmane Dembele. ***(Mundo Deportivo)***

### MATEO ANUKIA LEEDS

LEEDS United wamekubali dili la Espanyol katika kumsainisha mshambuliaji, Mateo Joseph Fernandez. ***(AS)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# TUCHEL NA SABABU KIPIGO CHELSEA KWA WEST HAM

●●● Kila mtu anahusika, tunaweza kulinda, lakini maamuzi pia hayakuwa bora kwa...

**LONDON,** England

KOCHA Mkuu wa Chelsea, Thomas Tuchel, amekiri kwamba Chelsea hawapaswi kuendelea kufanya makosa baada ya kichapo cha mabao 3-2 kutoka kwa West Ham United, Jumamosi.

Licha ya 'The Blues' hao kuongoza mara mbili, makosa ya kipa Edouard Mendy yaliwazawadia West Ham penalti, huku mlinda mlango huyo wa Senegal akishindwa kuzuia mpira wa krosi wa Arthur Masuaku kuingia ndani ya lango.

**Licha ya juhudi za kuusaka ushindi, na makosa ya wazi kutoka kwa Mendy, Chelsea ilifanya makosa mengine kadhaa kama timu, jambo ambalo Tuchel aliliitaja kwa haraka baada ya kumalizika kwa mechi.**

"Sidhani kama tulicheza vibaya, mechi ilikuwa sawa, tunaweza kushinda kwa uchezaji huu," alisema akiwaambia waandishi wa habari.

"Ni ngumu kucheza hapa, tulifanya makosa mengi ya binafsi. Tayari tulifanya dhidi ya Manchester United na Watford na tukaadhibiwa, ikiwa unataka matokeo katika kiwango hiki, lazima upunguze makosa."

Akizungumzia penalti ya kipindi cha kwanza, Mjerumani huyo aliongeza: "Kila mtu anahusika, tunaweza kulinda, lakini maamuzi pia hayakuwa bora kwa Edu katika hili."

CHEZA USHINDE KASINO

MECHI KALI
HOME AWAY
EVERTON
3.16 | 3.31 | 2.21
ARSENAL

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa vodacom m-pesa halopesa airtel money ZANTEL EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# XAVI: BAYERN LAZIMA WAKAE JUMATANO



**BARCELONA,** Hispania

KOCHA wa Barcelona, Xavi Hernandez, amesema anaamini timu yake inaweza kuifungua Bayern Munich kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya wiki hii licha ya kufungwa na Real Betis, Jumamosi.

Bao la dakika ya pili la Juanmi liliwezesha Betis kupata ushindi wa 1-0 kwenye Ligi Kuu Hispania, LaLiga, pale Camp Nou wakati Xavi akifungwa mechi yake ya kwanza tangu alipochukua nafasi ya Ronald Koeman, mwezi uliopita.

Mchezo huo wa Barca ni safari ya kwenda Munich Jumatano, ambapo ushindi utawafanya wafuzu hatua ya 16-bora ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Hata hivyo, sare au kipigo kitawafanya waondolewe na kutua kwenye Ligi ya Europa kama Benfica itaifunga Dynamo Kiev.

"Timu ina uwezo wa kwenda Munich na kushinda," alisema Xavi kwenye mkutano na waandishi wa habari baada ya mchezo dhidi ya Betis.

"Hilo ndio lengo letu. Tunajitegemea wenyewe. Tunakwenda kwenye moja ya viwanja vigumu sana duniani, lakini tunakwenda pale kujitoa kwa kila kitu na kuhakikisha tunashinda."



# *Ancelotti bado hafikirii ubingwa*

**MADRID,** Hispania

KOCHA Mkuu wa Real Madrid, Carlo Ancelotti, amesisitiza bado kuna safari ndefu ya kwenda Ligi Kuu Hispania, LaLiga, kwenye mbio za ubingwa baada ya 'Los Blancos' hao kujivuta kileleni kwa pointi nane.

Vinicius Junior na Luka Jovic walifunga kipindi cha pili wakati Madrid wakiwafunga Real Sociedad mabao 2-0 ugenini, Jumamosi.

Baada ya bingwa mtetezi, Atletico Madrid kufungwa mabao 2-1 na Real Mallorca mapema Jumamosi, kikosi hicho cha Ancelotti sasa kinaongoza kwa tofauti ya pointi 10 dhidi ya wapinzani wao hao wa jiji moja ambao watakutana Desemba 12, mwaka huu.

Hata hivyo, Ancelotti anajua bado kuna safari ndefu ya kwenda baada ya kucheza mechi 16.

"Nafikiri ilikuwa siku nzuri kwetu," alisema Ancelotti akiwaambia waandishi wa habari.


"Ligi bado ni ngumu na matokeo yameonyesha namna ilivyo ngumu na bado kuna mechi nyingi zinakuja, hivyo siwezi kusema kwamba sisi ni mabingwa.

LIVE IN PLAY

SPORTPESA APP

BET LEO UWE MILIONEA

PAKUA SASA



# MKWASA AWAANGUSHIA ZIGO WACHEZAJI KIPIGO NAMUNGO

**Na Dennis Fussi**

KOCHA Mkuu wa Ruvu Shooting, Boniface Mkwasa, amewatupia lawama wachezaji wake kwa kushindwa kuutumia vema uwanja wa nyumbani na kuruhusu kufungwa mabao 2-1 na Namungo.

Ruvu ilichezea kichapo katika uwanja wake wa nyumbani Ijumaa kwenye mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

**Akizungumza na mwandishi wetu, Mkwasa alisema hakutegemea matokeo hayo na hiyo imetokana na wachezaji wake kucheza kwa kujiamini kupita kiasi jambo ambalo limewagharimu.**

"Huu ulikuwa mchezo muhimu kwetu kuchukua pointi tatu hasa ukizingatia tulikuwa nyumbani, lakini mambo yamekwenda ndivyo sivyo, ndio mpira," alisema Mkwasa.

Aliongeza kusema kwamba, wachezaji wake waliingia kwenye mchezo huo wakijiamini sana, jambo ambalo anaamini liliwafanya kupoteza mchezo huo.

Kipigo hicho imeiacha Ruvu Shooting katika nafasi ya nane kwenye msimamo wa Ligi Kuu ikiwa na pointi tisa katika michezo nane iliyocheza mpaka sasa.



Waziri wa Utamaduni Sanaa na Michezo, Innocent Bashugwa, akiteta jambo na Mkurugenzi wa MultiChoice Tanzania, Jacqueline Woiso, wakati wa hafla ya MultiChoice Tanzania kuadhimisha maudhui ya ndani (Local Content Showcase) iliyofanyika mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam. Hafla hiyo iliambatana na uzinduzi rasmi wa tamthilia mpya za Danga na La Familia zinazoonyeshwa kupitia Chaneli ya Maisha Magic Bongo na Original Comedy, Watu Baki, Salama pamoja na Maskani Poa vinavyorushwa katika chaneli mpya ya Maisha Magic Poa. **NA MPIGAPICHA WETU**

# *Mennonite mshindi wa3 Umoja Cup*

**Na Mwandishi Wetu,** RORYA

TIMU ya Mennonite imeibuka mshindi wa tatu katika kinyang'anyiro cha michuano ya Umoja Cup 2021(ABEGA), wilayani Rorya baada ya Ijumaa iliyopita kuwashushia kipigo cha mbwa mwizi mabingwa wa msimu uliopita, Shirati Mji FC kwa kuwalaza mabao 5-2.

Mchezo huo wa kusaka mshindi wa tatu uliyopigwa katika Uwanja wa Maji Sota Ijumaa iliyopita, imefuatiwa na mechi ya fainali jana kati ya Wanamaji na Kirengo FC, ambayo imefunga michuano hiyo inayodhaminiwa na mdau mkubwa wa soka wa Rorya, Peter Owino, kwa mwaka wa tisa sasa.

Katika mechi hiyo ya kusaka mshindi wa tatu, licha ya kupigwa huku mvua ikinyesha, haikuweza kuzuia mashabiki kujitokeza kushuhudia mtanange huo mkali.

Mabao ya Mennonite mawili yalifungwa na Elliah huku Evanda Songo akifunga la tatu kwa shuti kali ndani ya 18.

Kipindi cha pili Shirati Mji walifanya mabadiliko ya kipa kwa kumtoa Michael na nafasi yake kuchukuliwa na Chile, lakini haikuweza kuwa sababu ya kuizuia Mennonite kuendelea kutabasamu kwa mabao kwani dakika ya 46 Mohamed Jumapili aliiandikia timu yake bao la nne kabla ya Evanda kurudi tena nyavu kuhitimisha ushindi huo wa mabao matano.

Kwa upande wa Shirati Mji ilipata mabao yake kupitia kwa Jerry huku wachezaji wa timu hiyo wakiendelea kuonyesha utovu wa nidhamu baada ya Barbara Nyandoto kupewa kadi ya njano dakika ya 40 kwa kosa la kutoa lugha isiyo ya staha kwa mwamuzi.

Owiti Jackson wa Shirati Mji pia alitolewa nje kwa kadi ya nyekundu baada ya kumchezea rafu mbaya Elia Boazm.

Kadi hiyo nyekundu kwa Shirati Mji ni ya pili kwani katika mchezo wa nusu fainali dhidi ya Wanamaji FC, nahodha wao, Omega Mwasi, pia alitolewa nje kwa kadi nyekundu kutokana na kuonyesha utovu wa nidhamu kipindi cha kwanza kwa kutoa lugha zisizo na staha kwa mwamuzi.


## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATATU - 06 - DESEMA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 1173 | Kirklarelispor vs Akhisar Bld | 1.91 | 3.42 | 3.51 |
| 13:00 | 3108 | Sanliurfaspor vs Pendikspor | 2.70 | 3.23 | 2.38 |
| 15:00 | 5165 | FK Graficar Beograd vs FC Rad | 2.88 | 2.83 | 2.50 |
| 15:30 | 3340 | Cherno More vs CSKA 1948 | 1.72 | 3.41 | 4.42 |
| 16:00 | 2825 | Radnik Surduluca vs FK Radnicki 1923 | 1.71 | 3.52 | 4.34 |
| 16:00 | 3189 | Crystal Palace U23 vs West Ham U23 | 2.14 | 3.94 | 2.65 |
| 16:00 | 4300 | Ipswich U23 vs Charlton U23 | 1.72 | 3.93 | 3.79 |
| 16:00 | 5315 | Cardiff City U23 vs Watford U23 | 1.35 | 5.02 | 6.18 |
| 18:00 | 2448 | Zaragoza vs Eibar | 2.56 | 2.95 | 2.85 |
| 18:00 | 3513 | Syrian Arab Republic vs Mauritania | 1.31 | 4.45 | 9.10 |
| 18:00 | 4807 | Tunisia vs United Arab Emirates | 1.57 | 3.80 | 6.20 |
| 18:30 | 5114 | Argesul Pitesti vs Gaz Metan Medias | 2.07 | 3.10 | 3.64 |
| 19:00 | 4824 | Stoke City U23 vs Southampton U23 | 2.05 | 3.52 | 3.04 |
| 20:00 | 1227 | Goeztepe vs Gaziantep BB | 2.30 | 3.31 | 2.96 |
| 20:00 | 1346 | Backa Topola vs Radnicki Nis | 2.14 | 3.28 | 3.04 |
| 20:00 | 2077 | Ethnikos Achnas vs Apollon Limassol | 5.74 | 3.96 | 1.55 |
| 20:00 | 2395 | Istra vs Slaven Belupo | 2.29 | 3.28 | 2.80 |
| 20:00 | 2405 | Sandecja vs OKS Odra Opole | 1.93 | 3.42 | 3.47 |
| 20:00 | 3015 | Konyaspor vs Yeni Malatyaspor | 1.71 | 3.80 | 4.44 |
| 20:00 | 3389 | Ankaragucu vs Balikesirspor | 1.19 | 5.76 | 11.53 |
| 20:00 | 3422 | Warta Poznan vs Wisla Krakow | 2.50 | 3.03 | 2.70 |
| 20:00 | 4950 | Menemen Bld vs Keciorengucu | 3.32 | 3.51 | 1.94 |
| 20:15 | 1381 | FC Cartagena vs Tenerife | 2.80 | 3.09 | 2.50 |
| 20:15 | 2536 | Chojnice vs ZKS Stal Rzeszow | 2.84 | 3.42 | 2.20 |
| 20:30 | 2531 | Lamia vs PAS Giannina | 2.77 | 3.01 | 2.62 |
| 20:30 | 3420 | Annecy FC vs Chateauroux | 2.19 | 3.23 | 3.13 |
| 20:30 | 3813 | Empoli vs Udinese | 2.55 | 3.35 | 2.70 |
| 20:30 | 5166 | SC Dnipro 1 vs Chernomorets Odessa | 1.34 | 4.83 | 6.76 |
| 21:00 | 1212 | Waldhof Mannheim vs Wehen | 1.95 | 3.48 | 3.58 |
| 21:00 | 1983 | West Bromwich U23 vs Middlesbrough U23 | 1.80 | 3.76 | 3.57 |
| 21:00 | 3934 | Aston Villa U23 vs Birmingham U23 | 1.63 | 4.06 | 4.15 |
| 21:15 | 2049 | Hapoel Haifa vs Hapoel Beer Sheva | 3.38 | 3.38 | 1.97 |
| 21:30 | 4202 | Botosani vs Universitatea Craiova | 3.64 | 3.20 | 2.03 |
| 22:00 | 1437 | Jong AZ Alkmaar vs SBV Excelsior | 3.23 | 3.82 | 1.95 |
| 22:00 | 1877 | Burnley U23 vs Nottingham U23 | 2.85 | 3.66 | 2.10 |
| 22:00 | 2309 | Jong PSV vs De Graafschap | 4.00 | 3.81 | 1.75 |
| 22:00 | 2362 | Oman vs Bahrain | 2.41 | 2.95 | 2.90 |
| 22:00 | 3737 | Newcastle U23 vs Sunderland U23 | 1.80 | 3.76 | 3.57 |
| 22:00 | 3845 | Jong Ajax vs Emmen | 2.49 | 3.66 | 2.43 |
| 22:00 | 4331 | Everton U23 vs Arsenal U23 | 3.32 | 4.05 | 1.81 |
| 22:00 | 5391 | Qatar vs Iraq | 2.27 | 3.04 | 3.04 |
| 22:00 | 5700 | Jong Utrecht vs ADO Den Haag | 3.85 | 4.00 | 1.74 |
| 22:45 | 1347 | Boreham Wood vs St.Albans | 1.58 | 4.06 | 5.15 |
| 22:45 | 1864 | Cagliari vs Torino | 3.16 | 3.21 | 2.31 |
| 22:45 | 5965 | Niort vs Toulouse | 4.52 | 3.44 | 1.76 |
| 23:00 | 1203 | Getafe vs Athletic Bilbao | 3.46 | 2.91 | 2.34 |
| 23:00 | 1739 | Girona vs Leganes | 2.42 | 2.95 | 3.05 |
| 23:00 | 1869 | Almirante Brown vs Barracas Central | 2.35 | 2.90 | 3.04 |
| 23:00 | 2343 | Everton vs Arsenal | 3.16 | 3.31 | 2.27 |
| 23:00 | 4386 | Avellino vs Bari | 2.55 | 3.19 | 2.75 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumatatu Desemba 6, 2021

Nipashe



Tuchel na sababu kipigo Chelsea

UKURASA 21

# Simba yatinga kutetea nafasi 4 Tanzania CAF

## ●●● Juhudi binafsi za Dilunga zashusha presha mashabiki, ikitinga...

**Na Adam Fungamwango**

NI rasmi sasa mabingwa wa nchi, Simba wamebeba dhamana ya kwenda kutetea nafasi ya Tanzania kuingiza timu nne kwenye michuano ya Shirikisho la Soka Afrika (CAF); Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho.

**Ikumbukwe hadi sasa Libya ina pointi sawa na Tanzania katika viwango vya CAF kwa nchi zenye sifa ya kuingiza timu nne kwenye mashindano yake kwa msimu ujao, hivyo kitendo cha Simba jana kufuzu hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho Afrika, kitaliwezesha taifa kuongeza pointi kadri inavyofanya vizuri katika michuano hiyo.**

Hata hivyo, Tanzania itakuwa katika mchuano mkali dhidi ya Libya ambayo inaitegemea Ali Ahli Tripoli kwenye Kombe la Shirikisho, ambayo jana usiku ilikuwa ikicheza dhidi ya Stade Malien ya Mali.

Wawakilishi hao wa Tanzania, Simba, licha ya jana kukubali kipigo cha mabao 2-1 dhidi ya Red Arrows kwenye Uwanja wa Mashujaa, Lusaka nchini Zambia walitinga hatua ya makundi kwa tofauti ya mabao 4-2 kutokana na ushindi wao wa Novemba 28, mwaka huu wa mabao 3-0 Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Timu hiyo sasa itasubiri droo ya michuano hiyo ili kujua itakuwa na timu gani katika kundi lake, hiyo ikiwa ni mara ya kwanza kwa Simba kucheza makundi ya Kombe la Shirikisho ingawa kabla ya mfumo huu mpya, ilishawahi kutinga hatua ya fainali na kufungwa mabao 2-0 Uwanja wa Taifa (kwa sasa Uhuru), Dar es Salaam dhidi ya Stella Abidjan, licha ya kutoka suluhu ugenini nchini Ivory Coast mwaka 1993.

Katika mchezo huo wa jana, wenyeji wakijua kuwa wana mlima mkubwa wa kupanda, waliianza mechi hiyo kwa kasi na dakika sita tu ya mchezo, Felix Bwalya alipiga shuti kali lililowababatiza mabeki wa Simba na kuiweka timu hiyo salama.

Simba ingeweza kuandika bao dakika ya tisa kama krosi safi iliyopigwa na Hassan Dilunga isingekoswa na Meddie Kagere, ambaye aliurukia kwa kichwa cha mbizi, lakini akapiga hewa badala ya mpira.

Rick Banda, ambaye alikuwa mwiba mchungu kwa Simba aliwaacha mabeki wa timu hiyo na kupiga krosi iliyounganishwa na Banda, lakini mpira ukatoka sentimita chache kwenye lango.

Dakika moja baadaye, Allasane Diara akiwa umbali wa mita 30, bila kukabwa na mtu yeyote aliachia kombora kali lililopita juu kidogo ya lango la Simba.

Dilunga tena, akiwa amehama upande, sasa akiwa kushoto alimwacha beki mmoja wa Red Arrows na kupiga krosi maridadi ambayo wachezaji wenyewe wa Simba, wakiongozwa na Kagere walishindwa kuuweka wavuni na kutoka kuwa wa kurushwa.

Kuanzia dakika ya 39, wenyeji walihamia kabisa kwenye lango la Simba na kufanya mashambulizi mfululizo, wakiongozwa na Kebson Kamanga hadi kufanikiwa kupata bao la kuongoza dakika moja kabla ya mapumziko.

Alikuwa ni Banda aliyefunga bao kwa shuti la kushutukiza lililojaa wavuni licha ya jitihada za Aishi Manula kujaribu kuokoa. Banda huyo huyo alifunga bao la pili kwa kichwa, dakika ya pili tu baada ya kipindi cha pili kuanza na kuwaweka roho juu wanachama na mashabiki wa Simba pamoja na Watanzania kwa ujumla waliokuwa uwanjani hapo na waliokuwa wanafuatilia kwenye televisheni na redio pia kwani wenyeji walihitajika bao moja tu ili mabao ya jumla yasomeke 3-3.

Baada ya presha ya mashambulizi kuwa kubwa, kocha Pablo Franco alimtoa Bernard Morrison na kumwingiza Shomari Kapombe kwenda kusaidia kukaba, lakini alikuwa ni Dilunga aliyekuwa kwenye kiwango bora jana, aliyerejesha uhai kwa Simba na kuwafanya wachezaji wa Red Arrows kunyong'onyea alipofunga bao dakika ya 66, lilionekana kumaliza mchezo mzima.

Zilikuwa ni juhudi zake binafsi alipompokonya mpira beki wa kushoto Tresor Tshibwabwa na kumzidi nguvu, akaingia nao ndani ya eneo la hatari na kupiga mpira kiufundi ukajaa wavuni na kumuacha kipa Charles Kalumba akishangaa.

Mbali na Morrison, Simba iliwatoa pia Kagere, Dilunga na Rally Bwalya, nafasi zao zikachukuliwa na John Bocco, Mzamiru Yassin na Joash Onyango.



Winga wa Simba, Hassan Dilunga 'HD', akiifungia timu yake bao pekee wakati wakikubali kipigo cha mabao 2-1 nchini Zambia dhidi ya wenyeji, Red Arrows, kwenye mechi ya mchujo ya Kombe la Shirikisho Afrika kuwania kufuzu hatua ya makundi. Simba imefuzu kwa tofauti ya mabao 4-2 kutokana na awali kushinda 3-0 nyumbani. **PICHA: SIMBA**

# Yanga 'mzuka wa dabi' juu

**Na Adam Fungamwango**

BAADHI ya wachezaji wa Yanga wameonyesha kuwa na hamu kucheza mechi ya 'dabi' dhidi ya watani wao wa jadi Simba, Jumapili wiki hii baada ya kuwataka wanachama na mashabiki wao kujitokeza kwa wingi kuangalia kitu watakachokifanya kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Wakizungumza jijini Dar es Salaam, wachezaji hao Mukoko Tonombe, Saido Ntibazonkiza na Heritier Makambo, wamekiri kuwa mechi itakuwa ngumu, lakini wao, Yanga wanachohitaji ni pointi tatu tu.

Simba na Yanga zitakutana Jumapili wiki hii kwenye mechi ya mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu Tanzania Bara inayoendelea nchini, ikiwa ni raundi ya nane.

"Mechi dhidi ya Simba ni ngumu, lakini tunafanya mazoezi kwa ajili ya kuchukua pointi tatu. Mimi nimejipanda kama ninavyocheza na timu zingine tu, nimeshacheza mechi kadhaa dhidi ya Simba kwa hiyo hainipi presha sana, ni kama nacheza dhidi ya Biashara United, Namungo na zingine," alisema Mukoko kiungo mkabaji, ambaye ana msimu wa pili kwenye klabu hiyo na amesh-acheza dhidi ya timu hiyo kwenye mechi za Ligi Kuu, Kombe la FA na Ngao ya Jamii pia.

Ntibazonkiza yeye alisema: "Mashabiki waje kwa wingi waangalie kitu ambacho wachezaji wao tutafanya siku hiyo."

Lakini kwa upande wa Makambo, ambaye amerejea tena msimu huu akitokea Horoya FC ya Guinea, alikiri kuwa mechi itakuwa ngumu, lakini kutokana na maandalizi yao mazuri watafanya vizuri, ila wanachohitaji ni sapoti ya wanachama na mashabiki wao.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31

9 770856 541002 >